

Adam Shafi Adam
Kuli
Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

Nacherzählt von
Lourenco Noronha
Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur
am
Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien
Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: Mai 2009

Widmung
Kutabaruku

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

Dibaji
Vorwort

Angeregt wurden diese didaktischen Unterlagen von Studierenden am Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien.

Die deutschsprachigen Teile wurden von Dr. Franz Rader korrigiert; dieser hat während seiner Tätigkeit an der Österreichischen Botschaft in Nairobi meine Berufung nach Wien gefördert. Für beides bin ich ihm dankbar.

Lourenco Noronha
E-mail: noronha@gmx.at

1. Utangulizi
Einleitung

Siehe die Einleitung zum Roman Kasri ya Mwinyi Fuad auf dieser Website
www.swahili-literatur.at

2. Matini
Texte

Majaliwa¹ ist ein Hafenarbeiter in Sansibar.

Wakati ana umri wa miaka hamsini na tano (mitano), Majaliwa alikuwa bado anafanya kazi ya ukuli. Kazi hii alianza wakati yungali kijana wa miaka ishirini na moja (mmoja). Mazoea ya kazi hiyo yalimfanya aimudu vizuri kabisa. Alikuwa mtu mashuhuri sana miongoni mwa wafanyakazi wa bandarini. Dongo la Majaliwa lilikuwa zuri sana kwani hata katika umri wa miaka hamsini na tano (mitano) alionyesha kama kijana wa miaka thelathini tu. Alikuwa na urefu wa wastani na mwingi wa mwili.

Majaliwa alikuwa mwingi wa heshima, lakini pindi alipokuwa kazini, aliziweka heshima hizo pembeni na kushika masihara na matusi kama ilivyo tabia ya makuli. Lakini palipotokea matatizo alikuwa ni mtu wa busara na mwingi wa huruma. Mara kwa mara aliwanasih wenzake waliokabiliwa na matatizo ya kinyumbani, wafanyakazi wengi wa bandarini walimhadithia Majaliwa ili awape nasaha na maongozi.

Majaliwa alikuwa na mkewe aliyeitwa Mashavu². Ijapokuwa Majaliwa na Bi. Mashavu walioana walipokuwa vijana, kwa muda mrefu walikuwa hawakubahatika kupata mtoto. Walikata tamaa ya kupata mtoto na hakuna mzimu walioubakisha tokea Unguja hadi Pemba katika jitihada za kuomba mtoto. Walipata mtoto wao wa kwanza na wa mwisho wakati wote wawili wameshakuwa watu wazima. Siku aliyozaliwa mtoto huyo, furaha ya wazee wawili hao ilikuwa haina kifani. Alikuwa mtoto mwanamume, wakampa jina la Rashidi³. (Uk. 1-2).

Majaliwa wohnt mit seiner Frau Bibi Mashavu und seinem Sohn Rashidi in Mfereji Maringo. Gewöhnlich steht er frühmorgens auf und geht arbeiten, doch an diesem einen Tag liegt er um 7.30 Uhr noch im Bett. Er ist krank. Seine Frau macht sich Sorgen um seine Gesundheit, aber auch um den Lebensunterhalt der Familie, denn ein Kuli ist ein Tagelöhner.

Majaliwa alikuwa hapendi kulala bila ya kwenda kazini kwa kuhofia mambo nyumbani yangukuwa mrama. Shilingi mbili ambazo alizipata kwa kutwa zilitumika kwa matumizi ya nyumbani isibaki hata senti moja. Na wala si kama pesa hizo zilitosha, bali ilimlazimu azifanye zitoshe. (Uk. 2).

Am folgenden Tag geht Majaliwa trotz seiner Krankheit arbeiten. Da an diesem Tag Eisenbahnschienen termingemäß abgeladen werden müssen, arbeiten die Hafenarbeiter durchgehend bis 18 Uhr.

Siku ya pili kazi ya kuteremsha vyuma vya njia ya reli iliendelea. Kila chuma kimoja, kama kawaida, kilichukuliwa na watu wanne.

„Chukua vizuri!“ Majaliwa ambaye alikuwa nyuma kabisa alimpiga kelele kuli mwenzake aliyeonyesha amelegea kidogo na ambaye alikuwa kati.

¹ *Ku-jalia* bedeutet „gewähren“, „gönnen“. *Nimejaliwa mema mengi Tanzania* bedeutet „Ich habe viel Gutes in Tansania erlebt.“ *Majaliwa* bedeutet „Gnadenerweis“, „Vorherbestimmung“, vielleicht auch „Jemand, dem viel Gutes gegönnt wurde.“

² *Shavu/ma-* bedeutet „Wange“. Vielleicht ist der Name Mashavu kein Kiswahili-Name.

³ *Rashid* bedeutet *wise, prudent, rightly-guided*. Siehe Koran surat Hud 11:87.

Walikibeba chuma hicho mpaka uwanjani vinapokusanywa vyuma vyote. Wakati wa kukitua chuma hicho iliwabidi wote wakitue kwa umoja wao.

„Tayari, tayari?“ aliuliza yule aliyekuwa mbele kisha akaamuru, „Haya tupa!“

Wote walikitupa kile chuma lakini kwa bahati mbaya yule aliyekuwa kati alichelewa kidogo na uzito wote wa chuma kile ukamwelelea yeye begani na mfupa wa bega lake la kuume ukadata.

„Aaaaa!“ akaanguka huku akipiga kelele nyingi kwa maumivu. Wafanyakazi wenzake na wengine waliokuwa karibu walimzunguka huku wakijaribu kumsaidia mfanyakazi mwenza aliyekuwa akipiga mikambe kama mtu mwenye kukata roho. Pale pale alikwenda kuitwa mkuu wa gati ambae (ambaye) alikuwa Mwingereza. Muda si muda alifika pale alipo majeruhi yule. Alimbonyeza bonyeza na kumfanya yule mfanyakazi azidi kupiga makelele kwa maumivu na mara yule Mzungu akasema, “Sasa peleka yeye nyumbani.”

„Tumpeleke nyumbani?“ Akida aliuliza. „Lazima tumpeleke hospitali, ameumia sana huyu,“ aliendelea.

„Nani tapeleka yeye hospitali?“⁴ Yule Mzungu aliuliza.

„Gari la kampuni si ipo?“ Wote waliopo pale walisema kwa umoja wao.

Yule Mzungu ambaye alikuwa amechutama huku alimgeuzageuza mjeruhi yule alisimama na kuwatazama wafanyakazi wale mmoja mmoja na kwa ukali alisema, “Nyinyi hapana jua kama gari ya kampuni iko kazi nyingi?”

„Muhimu hiyo kazi au huyu mtu aliyeumia? Unafikiri kazi muhimu kuliko maisha ya mtu?“ Akida aliuliza kwa hamaki.

„Hiyo hapana shauri yangu,“ alijibu yule Mzungu bila ya kumtazama yeyote katika watu waliokuwapo pale alikwenda zake. (Uk. 6-7).

Daraufhin übernimmt Majaliwa die Führung, macht eine Kollekte, mietet einen Wagen und bringt den Verletzten ins Spital. Sie alle wissen aber, daß er die Arbeit eines Kulis niemals wieder verrichten kann und einen anderen Beruf kennt er nicht.

Tag für Tag setzt Majaliwa seine Arbeit fort, bis er sie krankheitshalber ganz aufgeben muß. Bald darauf erliegt er der Krankheit und wird in der Nachbarschaft begraben. Seine Witwe ist nun Alleinverdienerin, die durch kleine Geschäfte den Lebensunterhalt der Familie zu bestreiten versucht. Rashidi hilft mit, indem er Speisen, die seine Mutter zubereitet, in den Gassen verkauft. Mit 16 Jahren geht er dann auf Suche nach Arbeit. So wie sein Vater will auch Rashidi ein Kuli werden. Schon um 7.30 Uhr morgens drängen sich - wie immer - Männer und Jungen am eisernen Tor des Hafens von Sansibar. Hier versucht auch der junge Rashidi, sich durchzusetzen.

Kelele, matusi na malalamiko, vijana, watu wazima na hata watoto, wote wakiwa wamevaa nguo chafu zilizoraruka, nyingine zikiwa zimepoteza rangi ya awali kwa kupauka na kwa kutiwa viraka vya rangi mbali mbali.

Nyuma ya mlango wa chuma amesimama Mhindi mmoja na vipande vya karatasi vya rangi ya kibuluu, anavigawa lakini kwa wale tu walio na nguvu, ya kuvinyakua kutoka mkononi mwake. Kila anapotoa kipande kingine mwitu wa mikono unakigombania.

⁴ In der Agitationsliteratur wird den Nicht-Afrikanern Kiswahili-Sprachkompetenz verweigert.

Hapa panatumika mabavu tu, hapana cha huruma wala utu. Lakini pamoja na mabavu hayo pana kujuana vile vile. Anayefahamiana na yule Mhindi mwenye kugawa vile vipande anaweza kukipata kipande kwa urahisi. Mhindi huyo anawaelewa wale wenye nguvu na walio mahodari kwa kazi za kichukuzi. Shida ni kwa wale wageni, wale ambao wamefika hapo kwa mara ya kwanza katika vita hivyo vya kutafuta kazi.

Hii ndiyo mandhari Rashidi aliyoikuta bandarini. Hapa ndipo baba yake aliponyonywa uhai wake akafa bila chochote. Unguja bandarini. Mwaka 1948. (Uk. 9).

An diesem ersten Tag gelingt es Rashidi nicht, eine blaue Karte zu ergattern. Er gibt nicht auf und geht weiter auf Suche nach Arbeit. Diesmal sucht er sie bei einem Araber, der Tagelöhner anstellt, die Säcke mit Kohle von den Schleppern abladen. Dieser Araber, ein Mshihiri⁵, spricht eine eigene Kiswahili-Variante.

Rashidi alimnyemelea yule Mshihiri kidogo kidogo huku akimwalia kutoka kichwani mpaka miguuni. Yule Mshihiri alikuwa na furushi la mabati mkononi na mabati hayo yalikuwa yamekatwa duara mfano wa shilingi na alikuwa akiyagawa mabati hayo miongoni mwa wale watu waliokuwa wakibeba vikapu vya makaa ya mawe.

„Washa maskhara yako weye, lazma kigapu nayaza tele,“ Mshihiri alimwambia mmoja wa wale wachukuzi ambaye kikapu chake hakikijazwa (hakikujazwa?) kama inavyotakiwa.

Mshihiri yule alikuwa mkali, jeuri na safihi. Alikuwa akitukana matusi mabaya mabaya akiwa anafanya mashihara na kweli humo humo. Wachukuzi walio majabari walimjibu na yeye akazidi kuwatukana kila walipomjibu. Rashidi alizidi kumsogelea huyu Mshihiri lakini kila alipotaka kumwambia neno alifanya hofu kwa kuchelea kutukanwa. Mwisho alijipa moyo akasema, „Eti Bwana ...“.

Yule mshihiri alimtazama kijeuri na mara akamwambia, „ya shekh, nini nataka haba, haba abana bahala ya mshezo.“ Yule Mshihiri alikuwa akisema huku uso amekunja. Kichwa kilikuwa kimezongwa kitambaa cheupe, uso umezungukwa na sharafa ya ndevu nyeusi na nyeupe ambazo kwa juu ziliungana na masharubu yake. (Uk. 13-14).

Rashidi geht ein wenig spazieren, beobachtet die Arbeiter und kommt wieder zu jenem Mshihiri.

„Eti Bwana mie naweza kupata kazi hapa!“ Kwa hofu Rashidi alimwuliza tena yule Mshihiri.

„Weye nataka kazi? Naweza kubeba kigabu ya makaa weye?“ Yule Mshihiri aliuliza huku akimbinyabinya mikono Rashidi.

„Naweza! N'tajaribu!“ Rashidi alijibu kwa sauti ya juu akiona ameshaitia kazi mkononi.

„Weye bado ndogo! Lenda zake yumbani! Weye habana soma skuli?“ (Uk. 14).

⁵ Die Araber, genannt *Mshihiri/wa-*, kamen aus Hadramaut, besaßen kleine Läden, arbeiteten am Hafen und verkauften gekochten Kaffee auf der Straße. Zu dieser unteren Schicht rechnete man auch die *Manga*-Araber (*Manga* ist in Kiswahili die Bezeichnung für die Gegend von Muskat), die ohne Kapital kamen, etwas Geld verdienten und wieder in ihre Heimat zurückkehrten. Weder die *Mshihiri* noch die *Manga*-Araber waren der Swahili-Sprache mächtig. Beide erlebten während der Volksrevolution den Zorn der Afrikaner unmittelbar.

Rashidi beobachtet im Stillen, wie der Mshihiri mit der Arbeitern umgeht, wie er sie beschimpft und wie er sie bezahlt. Rashidi zieht auf der Suche nach Arbeit weiter.

Er trifft einen Koch, der das Mittagessen für die Hafenarbeiter zubereitet und ihn für einen Tag anstellt. Rashidi hilft ihm, das Mittagessen zuzubereiten, zu servieren und das Geschirr abzuwaschen. Die Speisereste darf Rashidi als Lohn für seine Arbeit essen. Nach langer Zeit kann er sich einmal satt essen, hat aber immer noch kein Geld.

Am folgenden Tag geht er wieder auf Suche nach Arbeit. Obwohl er auch an diesem Tag keine bekommt, hat er doch Glück, denn er trifft Mzee Tindo, der eine kleine Gruppe von Hafenarbeitern leitet, die für die Clove Growers' Association (CGA)⁶ Gewürznelken ins Lager bringt. Mzee Tindo hat zu seinem Vorsteher, dem Inder Morarji gute Beziehungen, denn dieser bringt ihm fleißige und billige Arbeitskräfte. Mzee Tindo kennt Rashidi und dessen Eltern und ist bestrebt, ihm zu helfen und ersucht ihn, ihn in seiner Wohnung privat zu besuchen. Die Besprechung verläuft gut und Mzee Tindo ist bereit, Rashidi Arbeit zu geben.

Frühmorgens bevor die Sirene läutet, ist Rashidi beim Kino von Darajani, wo es ein Restaurant gibt. Dort trinkt er einen Kaffee und wartet auf Mzee Tindo, der rechtzeitig kommt und ihn in die Arbeit einführt. Obwohl Rashidi zu jung und zu schwach ist, Gewürznelkensäcke zu tragen, versucht er doch, die Arbeit zu verrichten. Es wird Feierabend. Mzee Tindo ruft die drei Arbeiter zu sich und teilt ihnen mit, daß er vom Arbeitgeber 15 Shilling erhalten hat. Er gibt jedem vier Shilling und drei behält er für sich selbst. Rashidi fragt sich, warum Mzee Tindo dieses Geld für sich behält, schweigt aber darüber.

Rashidi kehrt am Abend nach Hause zurück. Dort wartet seine Mutter, die das Abendessen zubereitet hat, auf ihn. Er gibt ihr zwei Shilling, zwei behält er für sich selbst. Für Bibi Mashavu ist ihr Sohn ihr einziger Hoffnungsträger und sie nennt ihn erfurchtsvoll „Baba“ (Uk. 22).

Bi Mashavu alikuwa jikoni anapakua chakula wakati Rashidi alipofika nyumbani. Wakati wa chajio ulikuwa umefika. Alipofika ndani Rashidi hakusema chochote ila aliingia chumbani mwake na kujilaza juu ya kitanda kidogo huku akijibenua kujinyosha viungo.

„Mbona nasikia parakacha parakacha huko! Nani tena huyo?“ Bi Mashavu aliuliza kutoka jikoni.

„Mie Rashidi.“

Bi Mashavu hakusema kitu, aliendelea na kazi yake. Alipakua chakula na kumtilia Rashidi chake.

„Baba chakula tayari.“

Rashidi ambaye kidogo usingizi ulimchukua kwa machofu aliyokuwa nayo alifungua macho akamwona mama yake amesimama mlangoni na sahani ya chakula.

⁶ Die CGA hatte das Monopol für den Ankauf aller Gewürznelken aus Sansibar und Pemba inne, die sie dann ins Ausland verkaufte.

„N'takula halafu, sasa napumzika kidogo,“ alijibu bila ya kuondoka pale kitandani.

Bi Mashavu alimwalia mwanawe na aliona dhahiri kwamba alikuwa amechoka sana.

„Mama chooni yapo maji?“ Rashidi aliuliza.

„Nilinunua 'maras' moja mchana basi nafikiri yangalimo,“ Bi Mashavu alijibu, Je! nikuletee maji ya moto?“ akauliza.

„Ya nini kupoteza kuni bure, n'takoga maji ya baridi,“ alijibu Rashidi.

Rashidi alizoa pale alipokuwa amelala. Akachukua taa ya kandili iliyokuwepo hapo katikati na kuingia chooni.

„Basi ukisha koga (kuoga) chakula kimo ndani ya kabati jikoni, mie nipo hapo nyumba n'nazungumza,“ Bi Mashavu alisema. (Uk. 42-43).

Rashidi geht jeden Tag an den gleichen Ort unter Aufsicht von Mzee Tindo arbeiten, möchte aber ein Kuli werden, so wie sein Vater es war.

Eines Tages, als Rashidi und seine Kollegen in der Mittagspause sind, wird das Thema Lohn wieder aufgegriffen. Von einem Mitarbeiter Farjalla⁷ erfährt Rashidi, daß Mzee Tindo einen Teil der Tageslöhne für sich behält und zusätzlich noch einen eigenen Gehalt kassiert. Rashidi schlägt seinen Kollegen vor, diese Situation mit Mzee Tindo zu besprechen. Als Rashidi am selben Tag bei der Auszahlung des Lohnes Mzee Tindo diese Beschwerden vorbringt, erkennt dieser die Gefahr und beschließt, daß zwei Arbeiter und er selbst die Belegschaft vor Morarji vertreten sollten. Die Arbeiter wählen Rashidi und Farjalla zu ihren Vertretern. In derselben Nacht geht Mzee Tindo heimlich zum Arbeitgeber, dem Inder Morarji⁸, und informiert ihn über das Vorhaben der Tagelöhner, wofür er eine Belohnung von zehn Shilling bekommt.

Am folgenden Tag gehen Mzee Tindo, Rashidi und Farjalla wie verabredet zu Morarji.

Morarji na mwenzake mmoja wa Kibaniani⁹ walikuwa wamekaa hapo ukumbini. Walikuwa wamekaa juu ya jukwaa lililotandikwa kwa mito iliyovishwa foronya nyeupe. Wote walikuwa wamejitawanya juu ya mito hiyo ambayo ilikuwa laini kabisa. Walivaa pia winda¹⁰ nyembamba ambazo hazikuweza kuwasitiri vizuri. Mbele yake Morarji palikuwa na sanduku zuri la msaji. Morarji na mwenzake walikuwa wanazungumza Kibaniani¹¹.

Mzee Tindo na wenzake walipofika mbele ya lango la nyumba hiyo walifanya hofu kuingia ndani, lakini Rashidi bila ya kujali kitu chochote ndiye aliyekuwa wa mwanzo (kwanza) kukiuka kizingiti cha lango hilo na kuingia ndani. Iliwabidi wenzake, yaani

⁷ Faraj bedeutet *comfort, ease, repose*. Vielleicht besteht Farjalla aus Faraj und Allah.

⁸ Das suffix *-ji* bei indischen Namen ist ein Ausdruck der Ehrerbietung.

⁹ Die *Banias* bzw. *Banyas* sind Geschäftsleute aus dem Teil-Staat Gujerat in Indien. Sie gelten in Indien als „*very shrewd*“.

¹⁰ Der Autor betont, daß Morarji und sein indischer Mitarbeiter ein *winda* tragen. Dieses Lendentuch, in Indien *lungi* genannt, wird von Afrikanern verachtet. Ein Sprichwort lautet: „*Ukimtaka Baniani umtake na winda wake*.“ Gemeint ist: „Wenn man etwas haben will, muß man auch dessen unangenehmen Seiten in Kauf nehmen.“ in der Swahili-Literatur zugeteilt wird.

¹¹ *Kibaniani* ist die Bezeichnung für eine Kiswahili-Variante einiger Inder in Tansania.

Farjalla na Mzee Tindo, wamfuate, na wote kwa umoja wao waliingia ndani na kukabiliana na Morarji uso kwa uso.

„Nin nataka hapa!“ Morarji aliwauliza kwa sauti ya kijeuri.

„Mukki! Si umesema tuje kukuona leo usiku,“ Mzee Tindo alijibu huku hofu imemjaa.

Morarji hata hakujali, aliendelea kuzungumza Kibaniani na mwenzake. Walizungumza kwa muda mrefu huku akina Rashidi wamesimama hapo mlangoni.

„Sasa nan nasema pesa hapana tosha? Wewe, wewe ... ?“ Morarji aliuliza baada ya kuacha mazungumzo yake akimwonyesha kidole Rashidi na Farjalla ili kutaka kumjua ni yupi hasa aliyesababisha matata. Farjalla alisimama kama hayupo, kimya kabisa, lakini Rashidi alijibu.

„Ndiyo mukki pesa kidogo, hazitoshi.“

„Nan mengine nasema pesa hapana tosha?“ Morarji aliuliza tena.

Wote walinyamaza kimya wamenywea kama waliotiwa maji. Rashidi mabega yalimpwaya alipohisi wenzake wamemtupa mkono.

„Basi kama wewe nasema pesa haitoshi kwenda tafuta kazi pahal ingine iko pesa mingi!“ Morarji alimwambia Rashidi kwa fedhuli, kisha alimgeukia Mzee Tindo na kumwambia, „Tindo! Hapana chukua yeye kazini tena, haya! Jao!“

Wote walitoka na kuelekea makwao.

„Kujua kwingi¹² huko, sasa unaona faida yake?“ Mzee Tindo alisema huku akimfanyia tashiti Rashidi.

Rashidi hakujibu kitu, alinyamaza kimya na kufuata njia yake moja kwa moja mpaka kwao. (Uk. 51-52).

Zwei Monate sind seither vergangen und Rashidi hat immer noch keine Arbeit gefunden. Die Geldnot daheim ist unerträglich, da seine Mutter wegen zunehmenden Alters nicht mehr arbeiten kann. Dazu droht der Hausbesitzer mit Kündigung, da sie sich mit der Bezahlung der Miete in Rückstand befinden. In dieser Notlage bittet die Mutter ihren Sohn, ihre Goldkette bei einem Pfandleiher zu hinterlegen und Geld auszuborgen. Sie öffnet ihre schöne alte Truhe, die aber jetzt mit Staub bedeckt ist, nimmt die Goldkette heraus und übergibt sie ihrem Sohn.

Alitoa kidani cha dhahabu ndani ya kasha hilo akampa Rashidi akipeleke kwa mwekaji rehani. Rashidi aliondoka nyumbani moja kwa moja mpaka Mlandege. Kutoka hapo mpaka Mchangani, Mbuyuni na Darajani, yako maduka ya Wahindi wawekaji rehani yaliyojipanga moja baada ya moja. Kila duka alilolitazama katika maduka haya lilikuwa limejaa watu wenye shida ya pesa wamekuja kuweka vitu vyo (vyao) rehani.

„Wanatudhulumu Wahindi hawa lakini haidhuru hakuna jambo lisilokuwa na mwisho!“¹³ Rashidi alijiambia nafsi yake. Chuki yake ilizidi alipofikiria ile siku walipokwenda kwa Morarji akafukuzwa kazi kama mbwa. (Uk. 53-54).

Er geht dennoch in ein Geschäft hinein, das nicht stark besucht wird.

¹² Sprichwort: „Kujua kwinyi kukosa mengi.“

¹³ Am Ende des Romans wird Rashidi ins Gefängnis geführt. Der Roman endet mit den Worten: „Yana mwisho haya.“

Mwishowe alifika kwenye duka moja la rehani lililokuwa peke yake hapo Darajani. Ndani ya duka hilo walikuwamo watu lakini si wengi. Walikuwamo watu sita waliokuwa wamekaa juu ya bao. Baniani mmoja alikuwa amekaa kwenye kiti ikiwepo meza kubwa mbele yake na pembeni mwa meza hiyo vilikuwepo vitabu vidogo vingi vilivyoandikwa kwa lugha ya Kihindi¹⁴.

Rashidi alikwenda mpaka mbele ya meza.

„Nimekuja na kitu changu nataka kukiweka rehani,“ alisema huku uso ameukunja. Alitia mfukoni na kutoa kifurushi kilichozongwa na kitambaa cheupe.

„Wewe hapana ona ile watu ingine nakaa juu ya bao?“ yule Baniani alisema, „nenda kaa pale juu ya bao mpaka nafika zamu yako,“ aliendelea.

Rasidi alikaa juu ya pembe ya bao na mmoja mmoja, wale watu waliomtangulia Rashidi walipeleka vitu vyao na kupewa pesa kama alivyopenda yule Baniani. Kila aliyepokea pesa alipewa cheti kilichoandikwa kwa lugha ya Kihindi. Ilipofika zamu ya Rashidi, alikichukua kile kifurushi na kukirusha juu ya meza ya yule Baniani.

„Fungua,“ yule Baniani alimwamuru Rashidi.

Alifanya kama alivyoambiwa na kutoka kwenye kifurushi hicho alitoa kidani kizuri cha dhahabu. Yule Baniani alikichukua kile kidani na kukiweka juu ya kiganja chake cha mkono wake na kupeleka juu na chini akijaribu kupima uzito wa kidani hicho. Karibu na vile vitabu pembeni ya meza palikuwa na kimizani kidogo, alikiweka kile kidani juu ya kile kimizani na upande wa pili wa kimizani hicho aliweka vijiwe vidogo vya shaba. Uzito wa vile vijiwe ulipolingana na uzito wa kile kidani alikiondoa kile kidani kutoka kwenye kile kimizani.

„Tapata shilingi mia¹⁵,“ alisema yule Baniani.

Huku uso ameukunja akihihi kwamba ile anayopitisha Baniani yule pale ni dhuluma tupu Rashidi alijibu, „haya lete.“

Rashidi alipokea kutoka kwa yule Baniani noti tano za shilingi ishirini ishirini na kama wenzake wote, alipewa kile cheti cheupe kilichoandikwa kwa lugha ya Kihindi.

„Lazima talipa faida ya shilingi kumi kila mwezi kama haikuja kugombo kwa haraka,“ yule Baniani alisema kwa jeuri.

„Ndiyo,“ Rashidi alijibu.

Alitoka nje ya duka hilo, na hakusimama pahala po pote mpaka kwao ambako alimkuta mama yake amekaa juu ya kile kitanda cha mayowe ukumbini.

„Nimepata shilingi mia,“ Rashidi alimwambia mama yake.

„Haizuri (haidhuru), tutalipa kodi ya nyumba na zitakazobakia zitatusaidia siku mbili tatu.“ (Uk. 54-55).

¹⁴ Die *Republic of India* besteht aus 26 Teil-Staaten mit Hindi als *National Language*, aber fast jeder Teil-Staat hat eine eigene State-Language.

¹⁵ In den 1970er Jahren entsprach ein Tanzania Shilling drei österreichischen Schilling. Der Fall Rashidi spielt sich um das Jahr 1948 ab.

Zum Glück bekommt Rashidi am folgenden Tag Arbeit als Kuli am Hafen. Er lernt Faraji kennen.

Siku ile kazi ilikuwa nyingi sana na kila aliyewahi kufika mapema mbele ya lango la chuma alipata kazi. Mpaka wakati huo kazi bado zilikuwepo.

Rashidi alisema kwa hofu, „Bwana! Mimi nimekuja kukuomba unisaidie kazi! Mimi n'na...“

„Ee! Faraji!¹⁶“ bila ya kumjibu kitu chochote Ramju alimwita mtu mmoja aliyekuwa akipita, „chukua hii toto peleka yeye kwenye gengi yako!“¹⁷

Faraji alimsogelea Rashidi na kumtazama akihusudu namna alivyoyumbika kiume.

„Kijana madhubiti lakini kula(?) ndogo. ... Twende huku,“ alimwamuru Rashidi.

Rashidi alijihisi kama mtu aliyeona nyota ya Jaha¹⁸. Mshangao aliokuwa nao ulizidi ile furaha iliyokuwa moyoni mwake. (*Uk.* 56-57).

Er verdient täglich fünf Shilling, drei davon gibt er seiner Mutter und zwei behält er für sich. Auch seine Mutter verdient ein wenig Geld durch Anfertigung von Matten für eine Firma.

Eines Tages kommt eine Schiffsladung aus England, die unter strenger Aufsicht von Herrn George¹⁹, einem Angestellten der Firma Smith Mackenzie, entladen wird.

Makuli walikuwa wanapakua masanduku ya bidhaa hizo muhimu na George, mkuu wa kampuni ya Smith Mackenzi, kampuni ya mabepari wa Kiingereza iliyomiliki gati ya Unguja amewasimamia pembeni. Alikuwa anang'ara, amevaa shati jeupe la mikono mifupi, suruali kipande nyeupe iliyotulia pasi kwa wanga iliyotiwa, soksi nyeupe zilizomfika mpaka magotini na viatu vya ngozi rangi ya chakleti vilivyong'arishwa vizuri; amesimama kwa mapozi mikono yake yote miwili kiunoni, anaamrisha tu. Alikuwa anakijua Kiswahili vizuri ila matamshi ya maneno ndiyo yalimshinda ikambidi ayatamke kama vile anavyotamka lugha yake ya Kiingereza.²⁰

„Hapana wacha sanduku naanguka wewe! Kamata na mkono mpaka sanduku nafika chini!“ George alitoa amri kwa sauti kubwa wakati kreni ya meli ilipokuwa ikinyanyua masanduku yaliyopakiwa ndani ya wavu mkubwa wa waya ulioning'inizwa kwa vikuku juu ya kreni hiyo. Wakati huo huo aliruka pale alipokuwa amesimama na kumsukuma kuli aliyekuwa karibu yake.

Kabla ya masanduku hayo kunyanyuliwa vizuri kreni iliteleza kidogo na yale masanduku yakaanguka sakafuni mwa meli ile. George alimpiga teke kubwa yule kuli aliyesimama upande ule uliojigonga na yule kuli alisinukia juu ya masanduku hayo.

¹⁶ „Faraj“ - ein arabisches Wort - bedeutet *comfort, relief, ease, repose*.

¹⁷ Der Autor lässt Ramju das Kiswahili-Soziolekt *Kibanyani* sprechen.

¹⁸ Ein Sprichwort: *Siku moja utapata kilango cha jaha*. Die Waswahili glauben, dass ein Stern namens *Jaha* ihnen Glück bringt.

¹⁹ George ist ein beliebter Name im britischen Königshaus.

²⁰ Die britischen Beamten mussten eine Kiswahili-Prüfung ablegen, bevor sie den Dienst in Ostafrika antraten. In diesem Roman wird ihnen Sprachkompetenz abgesprochen. Dies entspricht dem Stil eines Agitationsromans.

„Mimi nasema kamata sanduku mzuri wewe nacheza hapa!“, George, uso umemuiva, mwekundu kama papai jinsi kijua kilivyokuwa kikali. (Uk. 60-61).

An diesem Tag arbeiten die Kulis bis zum Abend durch ohne Mittagspause, ohne irgend etwas zu essen.

Siku hiyo kazi iliendelea tokea asubuhi mpaka saa moja ya usiku bila ya kumpumzika. Hapana aliyekula isipokuwa George aliyekuja melini humo na kifurushi kilichozongwa ndani ya mfuko wa karatasi. Ilipofika mchana George alikuwa akitoa ndani ya kifurushi hicho vipande vya mikate vilivyopangwa viwili viwili akila huku akiendelea na kusimamia kazi. (Uk. 61).

So wie sein Vater wird auch Rashidi von den Arbeitern geschätzt und geachtet. Er merkt, daß die Kulis hier nicht gleich gesinnt sind wie die Arbeiter von Mzee Tindo, denn diese Kulis sind ideologisch orientiert. Während der Pausen sitzen sie gerne in Gruppen und diskutieren ihre Lage.

„Hii kazi hii! Hii kazi ya kitumwa hii!“ alisema kuli mmoja siku moja walipokuwa wanapumzika juu ya sitaha ya meli walimokuwa wakifanya kazi.

„Hawa wanatutumia kama punda na kila tunapowambia habari ya nyongeza ya malipo wanatutia huku wakitutoa huku!“ aliongeza kuli mwingine. (Uk. 62).

Eines Tages kommt ein junger Mann²¹ zu den Kulis.

Siku moja hawakenda melini; walikuwa wakifanya kazi pale pale gatini. Punde alitokea kijana mmoja mfupi, amevaa suruali ya kitambaa kigumu cha kibuluu²², shati jeupe na viatu vya kanda na (katika) mkono wake wa kulia amechukua mfuko wa ngozi. Baada ya kumwona tu yule kijana, Faraji ambaye alikuwa akiongoza kazi alitoka kwenda kuonana naye. Faraji na yule mgeni walinong'ona kidogo na mara yule kijana alifungua mkoba wake na kutoa makaratasi na kumpa Faraji. Baada ya hapo walipeana mikono na kuagana. (Uk. 62).

Am folgenden Tag ist er wieder da. Diesmal geht er in das Büro des Herrn George, der für die Angelegenheiten der Firma Smith Mackenzie zuständig ist. Nach einer Besprechung, die eine Stunde dauert, kommen die beiden heraus, während sie noch in einen heftigen Wortwechsel verwickelt sind. Herr George steigt in sein Auto und fährt weg, Bakari geht seinen Weg und Faraji teilt Flugblätter aus, die er erhalten hat. Da Rashidi weder lesen noch schreiben kann, sucht er einen Freund - der Fak²³i heisst - auf, der ihm das Flugblatt vorliest. Die Hafendarbeiter fordern damit eine zusätzliche Bezahlung für Überstunden und Sozialversicherung.

„Sisi wafanyakazi wa bandarini tunadai tupatiwe nguo za kazi, vile vile tunadai kila mfanyakazi awe na dhamana kamili ya maisha yake, kwani mara nyingi hapa bandarini wafanyakazi wanafikiwa na ajali na kampuni haichukui hatua yo yote kuhusu maisha ya mfanyakazi anayefikiwa na ajali,“ Faki aliendelea. (Uk. 65).

Am folgenden Tag, als Herr George einen Kuli unter einem Baum schlafen sieht, packt er ihn am Kragen, hebt ihn auf und gibt ihm eine Ohrfeige. Der Kuli schlägt zurück,

²¹ Später erfährt die Leserin bzw. der Leser, dass er Bakari heisst. „Baker“ bzw. „Baqir“ – ein arabisches Wort – bedeutet „abounding in knowledge, erudite, learned“.

²² Jeans

²³ Faki entspricht sehr wahrscheinlich *faqih* - ein arabisches Wort - das *scholar* bedeutet.

doch bevor es zu einer Rauferei kommen kann, werden sie getrennt. Herr George beschimpft den Kuli „Bloody fool!“ (S. 68). Zum zweiten Mal beobachtet Rashidi, wie Herr George einen Kuli schlägt. Rashidi reflektiert:

„Bepari²⁴ ni bepari tu, akiwa Mhindi, Mzungu au kabila lolote lile.“ (Uk. 68).

Auf dem Heimweg kommen Faraji und Rashidi ausführlich auf die Arbeitsbedingungen zu sprechen.

Die Hafenarbeiter greifen jetzt zur Selbsthilfe. An einem Abend nach der Arbeit besuchen Faraji und Rashidi gemeinsam mit ihrem Freund Salum²⁵ Beni ein Haus, wo die Arbeiter lesen, schreiben und rechnen lernen. Rashidi, der nie in einem Schulzimmer gesessen ist, freut sich sehr und nimmt von nun an regelmäßig am Unterricht teil.

Zwischen den Arbeitern und der Firma Smith Mackenzie bahnt sich eine Auseinandersetzung an. Faraji warnt die Arbeiter vor Einzelaktionen und empfiehlt ein gemeinsames und wohlüberlegtes Vorgehen.

Faraji und Rashidi sind eingeteilt, Zucker aus einem Schiff aus Panama abzuladen. Während der Arbeit aber zerreißt das Seil eines Krans und die Zuckersäcke fallen herunter. Manafi²⁶, ein Kuli, wird von einem Sack getroffen und ins Meer geschleudert.

George alikuwa ofisini mwake sigara mdomoni.

„Manafi ametumbukia baharini na mpaka sasa hivi hatujamwona!“ Faraji akimwambia huku roho ikimwenda mbio.

„Naanguka menyewe au alikuwa melewa?“ George aliuliza.

„Kaanguka na gunia la sukari!“ Faraji alijibu.

„Sasa mimi nafanya nini?“ George aliuliza huku ameikamata sigara yake mkononi, amezungukwa na makaratasi yaliyokuwa juu ya meza yake. (Uk. 82).

Nach langen Verhandlungen gibt Herr George doch nach. Man sucht die Leiche, findet sie aber nicht. Für die Witwe und Waisenkinder Manafis hat die Firma nichts übrig, da er ein Tagelöhner war. Die Arbeiter protestieren und fragen sich, wie lange es noch dauern wird, bis sie einen Widerstand organisieren. Faraji fordert die Kulis auf, am kommenden Sonntagabend an einer Versammlung teilzunehmen und dort weitere Schritte zu beschließen.

Siku ya Jumapili, saa moja na nusu juu ya alama wafanyakazi wote wa bandarini walijijazana ndani ya kijumba kidogo pale Miembeni. Hiyo ndiyo ilikuwa ofisi ya wafanyakazi wa bandarini wa Zanzibar. Walikuwa wengi sana hata baadhi yao iliwabidi kusimama nje. Huu ulikuwa ni mkutano wa kwanza kwa Rashidi kuhudhuria na siku hiyo ndipo alipojua kwamba kumbe wafanyakazi wa bandarini walikuwa wana chama chao madhubuti.

²⁴ „Bepar“ auf „Indisch“ bedeutet: Ladeninhaber, „Shopkeeper“. Nach der Einführung von *Ujamaa* im Jahre 1967 hat das Wort *bepari* 5/6 in Kiswahili die gegenwärtige Bedeutung von „Kapitalist“ bekommen.

²⁵ Vielleicht ist *Salum* eine Variante von *Salim* - ein arabisches Wort - das *perfect, complete, safe, secure* bedeutet.

²⁶ Manaf, bzw. Abd Manaf war ein Vorfahre des Propheten Mohammed (*Sifa nyingi zimwendee juu yake!*)

Siku hiyo Rashidi alimwona tena yule kijana aliyekuwa akimwona kule gatini na mfuko wa ngozi akija kuzungumza na Faraji. Siku hii ilikuwa (alikuwa) na mfuko wake ule ule. Baada ya kumwona tu Rashidi alikumbuka siku ile yule alipopigizana kelele na George ofisini mwake.

Kijana yule aliitwa Bakari²⁷. Aliingia ndani na kukaa juu ya kiti. Pembeni pale alikaa Faraji. Pia palikuwa na watu wengine wawili waliokaa juu ya viti. Watu hao nao Rashidi aliwajua kwa kuwaona kule pwani tu.

Bakari na Faraji walinong'ona na mara Bakari alifungua mkoba wake wa ngozi na kutoa makaratasi. Aliyasoma kimya baadhi ya yale makaratasi aliyoyatoa na halafu alisimama. Wafanyakazi wote walinyamaza kimya kumpa nafasi ya kusema, naye akaanza. (*Uk. 83-84*).

Bakari hält eine Ansprache, die den späteren Streik einleitet.

„Ndugu wafanyakazi wa bandarini. Leo tumekutana hapa ili kuzungumzia mambo muhimu yanayohusu maisha yetu. Kwa miaka mingi sasa mabepari wamekuwa wanatuchezea na kila tunapopeleka madai yetu wao wanatuona sisi wapumbavu. Wenzetu wengi wamepoteza maisha yao wakiwa kazini na wengine mpaka hii leo wana vilema kwa sababu ya ajali zilizowapata wakiwa kazini. Hivi juzi tu mwenzetu mmoja amepoteza maisha yake na kampuni ya *Smith Mackenzie* inasema wao hawana shauri lolote kuhusu marehemu huyo. Sasa ndugu wakati umefika tuchukue hatua, au vipi ndugu?“

„Ndiyo!“ Watu walipiga kelele kwa umoja.

„Sasa ndugu silaha yetu kubwa tuliyo nayo ni kuitisha mgomo. Je! tuko tayari kugoma?“

„Tuko tayari!“ Wote walijibu tena.

„Basi tunakarifuni (*andere Formen*: tunawaarifu nyinyi, tunawaarifuni) rasmi kwamba kesho tunaanza mgomo na hapana ruhusa mfanyakazi hata mmoja wa bandarini kwenda kazini.“

Bakari aliendelea na hotuba yake na alieleza mipango kadha kuhusu mgomo wao lakini kabla hajawahi kumaliza, bila ya wao kujua, yalifika magari mawili ya polisi na kiasi cha askari kumi na mbili (wawili) waliteremka (walitelemka) kutoka mwenye magari hayo. Askari waliongozwa na afisa mmoja wa Kiingereza. Wote walikuwa wamechukua virungu.

Walipotemka tu wale askari, watu wote ambao walikuwa wakisikiliza mkutano pale nje walitawanyika na kukimbia. Askari hao, virungu mkononi waliingia moja kwa moja mpaka ndani ya ile ofisi ambamo mkutano ulikuwa ukiendelea. (*Uk. 84-85*).

Der Saal, wo die Arbeiterversammlung stattfindet, ist gesteckt voll. Es entsteht ein Wirbel, die Teilnehmer versuchen zu flüchten, während die Polizei auf sie mit Schlagstöcken einprügelt. Danach dringt die Polizei zum Tisch vor, wo Faraji und Bakari die Versammlung leiten. Ein britischer Polizeioffizier versucht, die Ledertasche Bakaris wegzunehmen, aber Rashidi kommt ihm zuvor und verschwindet damit. Der Offizier fordert Faraji und Bakari auf, die Genehmigung für diese Versammlung vorzuweisen. Bakari möchte aber von ihm wissen, warum er zuerst die Teilnehmer schlug und erst jetzt die Bewilligung verlangt. Faraji wendet dazu ein, daß es eine

²⁷ Erst jetzt erfährt man seinen Namen.

vereinsinterne Versammlung ist und man daher keine Bewilligung braucht. Der Offizier läßt beide verhaften und einsperren. Rashidi geht rasch nach Hause, versteckt die Ledertasche und kommt zurück. Die Versammlung ist aufgelöst, niemand ist zu sehen, außer jene, die ihre Zeit für gewöhnlich mit Kartenspielen vertreiben.

Viele Arbeiter und Sympathisanten haben sich vor der Polizeistation Ng'ambo versammelt, wo Faraji und Bakari eingesperrt sind. Sie ziehen sich aber zurück, als die Polizei mit Waffengebrauch droht.

Boten gehen durch die Gassen und informieren die Arbeiter über den bevorstehenden Streik. Die Nachricht verbreitet sich rasch unter allen Arbeitergruppen. Am Streiktag ist Ramju da, aber niemand verlangt nach seinen blauen Zetteln. George und andere Beamte sind auch da, doch die Arbeiter bleiben aus. Die Firma Smith Mackenzie ist zum ersten Mal mit einem Streik auf Sansibar konfrontiert. Die Kolonialbeamten sind fassunglos. Sie versuchen, die Arbeiter zu überreden, die Arbeit wieder aufzunehmen. Die Arbeiter aber beharren auf der Erfüllung ihrer Forderungen.

Faraji und Bakari befinden sich noch in Untersuchungshaft.

Mara kwa ghafla walisikia milio ya funguo na lango la chuma la chumba walichotiwa lilifunguliwa. Walimwona askari amewasimamia mbele yao na kuwaambia, „Tokeni mnahitajiwa huku.“

Walitoka na yule askari aliwaongoza mpaka ndani ya chumba kimoja. Humo walimkuta afisa mwingine wa Kiingereza. Alikuwa amekaa juu ya kiti, mnene kama kiboko²⁸. Meza iliyokuwa mbele yake ilikuwa imejaa makaratasi. Alikuwa amevalia sare ya kaki ya polisi iliyotulia wanga.

Baada ya kuingia tu Bakari na Faraji aliwatazama kwa hasira na kuwauliza, „Ninyi nataka matata?“

„Sisi hatutaki matata lakini ninyi nd’o mnotaka (mnaotaka) matata,“ Faraji alijibu huku roho yake tanda bila mashaka wala taharaki.

„Leo lazima watu yote nakwenda kazini,“ alisema yule afisa wa Kiingereza²⁹ kwa hamaki.

„Huwezi kutulazimisha kufanya kazi kwani hilo ni jambo la hiyari (hiari) yetu,“ Faraji alijibu kwa ukaidi mdomo ameukaza kwa ghadhabu.

Bakari alikuwa amenyamaza kimya anaangaza huku na huku mle ndani ya ofisi iliyokuwa imepambwa kwa mapicha mbali mbali ya maafisa wa polisi wa zamani wa Kiingereza.

„Sasa ninyi kama hataki rejesha watu kazini serikali itashtaki ninyi,“ yule afisa wa Kiingereza lipaza (alipaza) sauti.

Pale pale aligonga kengele iliyokuwa mbele yake juu ya meza na kiasi cha kufumba na fumbua alifika askari na kusimama sawa halafu akatoa saluti.

„Rejesha wao ndani!“ yule afisa aliamuru.

„Timam afande!“ alijibu yule askari na mara aliwachukua Bakari na Faraji na kuwarejesha katika chumba kile kile walichokuwamo. (Uk. 89-90).

²⁸ Diese Beschreibung eines Kolonialbeamten ist ein Aspekt der Agitationsliteratur.

²⁹ Auch diesem britischen Beamten wird Sprachkompetenz verweigert.

Die Arbeiter selbst wissen nicht, wie es weitergehen soll. Sie haben sich im Vereinslokal versammelt und warten auf weitere Anordnungen. Chum, ein Abgeordneter, ersucht sie, nach Hause zu gehen und das Ergebnis der Besprechung mit dem Polizeidirektor in Beit-el-Ajaib³⁰ abzuwarten. Chum, Ubwa und Mbaraka³¹ fahren auf ihren Fahrrädern zur Polizeidirektion, werden vom Polizeidirektor empfangen, der nich "Listen you fools" belastet. Er geht auf ihre Forderungen nicht ein. Am dritten Streiktag beschließt ein Ausschuß noch eine Delegation zur Polizeidirektion zu schicken, die die Freilassung von Faraji und Bakari fordern soll, was ihnen auch gelingt.

Den Arbeitern geht es schlecht, aber auch die Firma Smith Mackenzie beginnt die Folgen des Streiks zu spüren und ist bereit, mit den Arbeitern zu verhandeln. Die Verhandlungen finden im Konferenzzimmer des Hauptsitzes der Firma statt³². Vier hohe britische Angestellte vertreten die Firma, während Faraji und Bakari im Auftrag der Arbeiter sprechen.

Waingereza wanne, wote wakuu wa kampuni ya Smith Mackenzie, walikuwa wanawangojea Bakari na Faraji ambao walifika kiasi cha saa tatu asubuhi.

„Well, get them some tea,“ alisema mmoja katika wale Waingereza. Pale pale mwingine alinyanyua simu iliyokuwapo pale juu ya meza na kuzungumza na mtu kwa lugha ya Kiingereza. Haikuchukua muda aliingia msichana mzuri wa Kihindi akiwa amechukua chano kilichojaa vikombe vya chai. Aliviweka vile vikombe mbele ya kila mmoja katika watu waliokuwamo chumbani mle na baada ya kumaliza tu kazi hiyo alitoka nje kwa mapozi³³.

Kwa siri Faraji alimkanyaga mguu Bakari na kuubonyeza mguu huo aliomkanyaga na kwa chati. Bakari alimtizama (alimtazama) Faraji.

„Karibu chai,“ mmoja katika wale Wazungu alisema huku yeye mwenyewe amenyanyua kikombe chake na kuanza kunywa.

„Sisi hatukujia chai hapo,“ Bakari alijibu. „Uncivilized people!“ alisema yule Mzungu huku akipiga funda la chai. „Ha! Ha! Ha!“ Wazungu wote wengine walicheka kwa umoja wao.

Bakari alielewa Kiingereza vizuri lakini hakutaka kusema kitu.

³⁰ „Haus der Wunder, Wunderschönes Haus“: der Amtssitz der Regierung, Sultanspalast.

³¹ „Barakat“ ist ein arabisches Wort. Es bedeutet „blessings, good fortunes, prosperities“.

³² Abgesehen von der üblichen Sprachinferiorität und Sprachinkompetenz der Europäer, wenn es um Kiswahili geht, stellt der Autor im folgenden Text dem Leser einige britische Verhaltensweisen zur Kolonialzeit vor, zu denen Tee und Diplomatie gehörten.

³³ Ist diese graziöse Inderin, die Tee serviert, als angenehmer Ausgleich gedacht zu den indischen Pfandleihern, dem groben Ramju am Hafentor und dem rücksichtslosen Morarji gedacht?

„Let's see who will bell³⁴ the cat,“ alisema mmoja wao wote wakiwa katika hali ya furaha na vikombe vyao vya chai mikononi.

„Sasa nini shauri? Watu takwenda kazini au hapana?“ aliuliza yule Mzungu aliyekuwa akivuta kiko.

„Hawaendi!“ Faraji alijibu.

„Sababu gani?“ aliuliza tena yule Mzungu.

„Sababu gani?“ Faraji aliuliza bila wasiwasi, „sababu mnaijua vizuri,“ aliendelea.

„Sikiliza!“ alianza yule Mzungu ambaye alikuwa anakabiliaana uso kwa uso na Faraji,

„Unajua kama nyinyi hapana kutaka kufanya kazi iko watu mingi hapa mjini naranda ovyo kama mbuzi na sisi naweza chukua wao kazini.“

„Tunajua,“ alijibu Faraji, ametulia moyo wake tanda kabisa.

„Come on, not like that Morris!“ Yule Mzungu mwingine ambaye alikuwa akivuta kiko alimwambia mwenzake kama kumtaka atumie lugha ya upole.

„Sikiliza,“ alianza kusema yule mwenye kuvuta kiko, kiko chake amekiweka juu ya kisahani cha kutupia jivu sigareti, mikono yake ipo juu ya meza. Vidole vyake vya mkono na kushoto amevipitisha ndani ya vidole vya mkono wa kulia,

„Sisi tokea zamani nataka ongeza ninyi pesa lakini *company* kila siku napata hasara,“ aliendelea.

„Mnapata hasara nyie?“ Bakari ambaye alikuwa amekaa kimya aliingia kati, „Kama mnapata hasara ya nini basi mnaendelea na kuwapo hapa hamfungi kampuni mkarejea makwenu?“ aliendelea.

„Sasa ninyi nataka pesa ngapi?“ aliuliza yule Mzungu.

„Sisi hatutaki pesa tu, kuna mengi tunayoyataka na yote tumekuleteeni katika madai yetu,“ alisema Faraji.

„Basi sisi tafikiri madai yenu kidogo kidogo wala hapana haja nyinyi nagoma. Wambie watu yote nakwenda kazini na sisi natengeneza kila kitu kidogo kidogo, right?“ alisema yule Mzungu.

„Na yule mwenzetu aliyekufa kazini?“ aliuliza tena.

„Habari yake pia sisi tafikiria,“ alijibu yule Mzungu.

Mazungumzo yaliishia hapo. Faraji na Bakari waliondoka baada ya kupewa ahadi kwamba madai yao yatafikiriwa na kwa siku ya kumi tokea kuanza mgomo kazi illanza tena huko gatini. (Uk. 94-96).

Am zehnten Tag nach Ausbruch des Streiks kommen die Hafenarbeiter wieder zur Arbeitsstelle, nehmen die Arbeit aber nicht auf. Die Tage vergehen. Die Arbeiter warten vergeblich auf die Erfüllung ihrer Forderungen.

Rashidi bringt wieder zwei goldene Armringe, die seiner Mutter gehören, zu einem Pfandleiher, nimmt ein Darlehen auf, um die finanzielle Notlage in der Familie zu überbrücken und geht wieder zur Arbeit. Die Arbeiter sind finanziell gezwungen, den Streik aufzugeben.

Eines Tages um die Mittagszeit kommt Herr George und bittet Rashidi, sofort mit einem Nachbar, der ihn sucht, nach Hause zu gehen. Dorthin kommend, sieht Rashidi, daß seine Mutter im Sterben liegt. Ihre Augen sind offen, sie kann aber kein Wort sprechen.

³⁴ Es ist eine historische Tatsache, daß ein Colonel Bell, Commissioner of Police, für die Freilassung von zwei Männern, die bei diesem Streik verhaftet wurden, verantwortlich war. Ist aber die Redewendung: „ (...) *who will bell the cat*“ (S. 95) hier ein Zufall?

Er geht rasch hinaus, um Hilfe bei Nachbarn zu holen, doch als er nach Hause zurückkehrt, ist die Mutter schon tot.

Siku ya pili baada ya sala ya alasiri Bi Mashavu alizikwa.

Kifo cha Bi Mashavu kiliwacha pengo kubwa katika maisha ya Rashidi. Kwa mwezi mmoja wa kwanza baada ya kifo cha mama yake Rashidi alikonda na kupoteza umbile lake la kawaida lakini kila siku zilivyoendelea majonzi yalizidi kumpungua mpaka akarejea hali yake ya kawaida. (*Uk. 100*).

Rashidi steht nun allein da, ohne Geld und ohne Geschwister. Er hat aber einen Onkel Mzee Farhani³⁵, den er besucht und der, zusammen mit einigen Hafenarbeitern, ihm beim Begräbnis seiner Mutter hilft.

Rashidi ist nicht nur allein, sondern auch einsam und sucht Anschluß. Ein Arbeitskollege Salum lädt ihn eines Abends ein, ein Taarab-Lokal zu besuchen.

Kwa upande wa pili wa watu waliokuwa wakitazama taarab Rashidi alimwona tena yule msichana aliyemvutia sana kule benini na ambaye alikuwa kama samaku kwa macho yake na hapo hapo alimtikisa Salum na kumwuliza, „Halo, unamjua yule mtoto?“

„Yupi?“

„Yule!“ Rashidi alinyosha kidole upande wa yule msichana.

„E-e-nishamwona, ana nini?“

Rashidi hakujua la kujibu. Alibaki kuguna tu.

„Ana nini? Mzuri yakhe!“ Salum alisema kwa hamu ya kutaka kujua zaidi.

„Hebu twende kule!“ Rashidi aliamuru huku akimvuta mkono Salum bila ya kujali kama amekubali kwenda kule anakotaka yeye au la. Wanaondoka pale na kuanza kupigana vikumbo na maashki wa taarab mpaka wakafika pale alipo yule msichana.

Baada ya kufika tu huku beni ilianza tena na yule msichana alipousikia mlio wa beni aligeuka ghafla ili kukimbilia benini. Wakati alipogeuka kwa ghafla akiwa yumo katika haraka ya kukimbilia benini alimpiga kikumbo Rashidi aliyekuwa nyuma yake. Rashidi alimzuia kwa mikono miwili kama kutaka kumkumbatia. Alimtazama machoni lakini kabla Rashidi hajawahi kusema kitu yule msichana alimwuliza hali, „Hujambo?“

Kabla Rashidi hajajibu, msichana alivuka kundi la waliokuwa wakitazama taarab, moja kwa moja mpaka kwenye beni. (*Uk. 105-106*).

Er macht einen Annäherungsversuch.

„Ulisikia niliyokuambia?“

Yule msichana alilegeza mwendo huku akijidai kutizama (kutazama) chini kwa kuona haya akauliza, „Unasemaje?“

Salum alikaa kwa mbali akiwafuata Rashidi na yule msichana kidogo kidogo. Wasi wasi ulikuwa umemjaa Rashidi, hajui aanze nini katika mazungumzo yake.

„N-nataka kukuuliza kitu!“

„Kitu gani?“

„Jina lako nani?“ Rashidi aliuliza kwa pupa.

„Amina³⁶,“ alijibu yule msichana.

³⁵ „Farhan“ ist ein arabisches Wort. Es bedeutet „glad, happy, cheerful, delighted“.

³⁶ Amina bedeutet *trustworthy, honest*

„Naona kama nakukumbuka?“ Rashidi aliuliza akiwa ameshazishinda hofu na wasi wasi aliokuwa nao.

„Mimi nakuona kila mara hapo Gulioni,“ alisema Amina.

„Kwani wewe unakaa Gulioni?“ Rashidi aliuliza kwa hamu.

„Ndiyo.“

Amina alikuwa anazungumza kwa heshima na upole huku uso wake ameuinamisha chini anacheza vidole vyake vya mikono.

„Unakaa Gulioni pahala gani?“ Rashidi aliuliza.

„Ah“ Hata sijui nikwelekeze vipi! Unaijua ile nyumba yenye mtufaa ndani uani?“ Amina aliuliza.

Rashidi aliinama kidogo kufikiri na mara aliinuka na kusema “E-e-e-e! Naijua! Ala! Unakaa nyumba ile wewe?“

„Siyo nyumba ile,“ alianza Amina, „baada ya nyumba ile ya pili ya tatu, ya nne yake.“

„Aaaa! Nishaijua nyumba yenyewe,“ alisema Rashidi na mara akauliza kwa ghafla, „yule Mzee Tindo bado anakaa mle mle?“

„Babu Tindo?“ aliuliza Amina, „Yumo mle mle lakini siku hizi si mtembezi,“ aliendelea.

Rashidi hakutaka kuenedeleza mazungumzo kuhusu Mzee Tindo. (*Uk. 109*).

Sie stimmt einem Termin für ein erstes Treffen zu. Für beide ist es die erste Liebe. Nach dem ersten Treffen kommen sie wieder von Zeit zu Zeit zusammen. Als er seinen Wunsch äußert, sie zu heiraten, lehnt sie den Wunsch nicht ab.

Amina aliinamisha uso chini, haya zimemjaa huku akifikiri la kujibu au kuuliza. Alibakia vile vile uso chini kwa muda bila ya kuweza kusema kitu cho chote.

„Je? Unasemaje umekubali?“ Rashidi aliuliza.

„Unakusudia kusema kwamba unanitaka siyo?“

„Ndiyo,“ Rashidi alijibu kwa haraka.

„Kama unanitaka basi njoo kwetu kwa wazee wangu uje kuniposa.“

„Hilo ni jambo litakalofuatia baadaye, kwanza nijibu kama umekubali kupendana na mimi au la.“

„Ah! Ninyi wanaume wa siku hizi hamna mwamana. Mnajidai mnapenda kumbe hampendi chochote huwa mnataka kumharibia mtu maisha yake tu. Mkishapata mnalolitaka mnakimbia,“ Amina alisema, akiwa mara hii uso hautazami chini bali anamtazama Rashidi machoni moja kwa moja.

„Mimi nakuahidi sitokuwa (sitakuwa) hivyo,“ Rashidi alisema akiwa amemsogelea Amina karibu zaidi na kuanza tena kumkamata mikono.

„Wanaume wote husema hivyo, hutoa kila ahadi wanapotaka lao lakini inapodhihiri kweli huruka huko! Sina haja ya kwenda mbali, jirani yetu pale, yule mtoto anaitwa Zainabu, alikuwa na rafiki yake aliyemdanganya kama atamwoa. Mwenyewe alikuwa akijinata kama kapata mchumba, wakifuatana masenema (masinema), jioni wakitembea pamoja, na mambo hayo yaliendelea mpaka kuchukua mimba na baada ya kuzaa tu mchumba kakimbia hamwulizi kheri (heri) wala shari³⁷. Hata pale karibu na kwao siku hizi hapiti; basi mimi hayo sitaki.“ (*Uk. 111-112*).

Rashidi ist ein Gelegenheitsarbeiter. Er hat noch keine Ersparnisse, kann auch keine Familie ernähren.

³⁷ Redewendung

Salum und Rashidi sind Freunde geworden. Sie verbringen ihre Freizeit gemeinsam in Tanz- und Schanklokalen. Als sie eines späten Abends betrunken am Haus Aminas vorbeigehen, ruft Rashidi diese laut beim Namen.

Alipofika mlangoni alimkuta Rashidi ameegemea mlango hawezi kujizuia.

„Ahh! Amina mpenzi wangu! Mimi nna...“

Rashidi hakuwahi kumaliza maneno yake mara kwa sauti ya hamaki Amina alisema, „Oh! Wewe Rashidi unathubutu kufanya hivyo! Sijakufikiria hata kidogo! Umenifuatia kwetu ilhali umelewa namna hiyo! Umekusudia kuja kunivunja heshima yangu siyo?“

„Amina njoo nikwambie mara moja,“ Rashidi aliendelea bila ya kujali yote yale aliyoyasema Amina.

„Sitaki! Nenda zako mhuni mkubwa we! Toka nenda zako.“ (Uk. 122-123).

Er hat Glück, daß sie allein zu Hause ist und niemand etwas davon erfährt.

Eines Tages, als es stark regnet und die Kulis trotzdem arbeiten gehen, kehrt Rashidi verkühlt nach Hause zurück und legt sich sofort schlafen. Kurz darauf hört er eine Stimme, die um Einlaß bittet. Er erkennt die Stimme Aminas und freut sich. Er heißt sie herzlich willkommen. Nach einer kurzen Begrüßung gibt sie ihrer Enttäuschung Ausdruck, daß er ein Trinker ist. Er erklärt ihr, daß es ein einmaliger Fall war und bittet um Entschuldigung. Sie fragt ihn schüchtern, ob er sie wirklich liebt.

Pale pale Amina aliyageuza maneno na kumwuliza Rashidi, „Lakini wewe Rashidi unanipenda kweli au unataka kunizuzua tu?“

„Amina,“ Rashidi alianza kusema, „si kitu ninachoweza kukuonyesha lakini laiti kama pendo lingeweza kuonekana basi lingelikuonyesha pendo langu juu yako. Mimi nakupenda, tena sana. Maneno kama haya sikuwahi kumwambia mwanamke ‘nakupenda’, wewe ndiye wa mwanzo (kwanza).“

„Kweli Rashidi?“ Amina aliuliza kwa sauti ya chini.

„Amini³⁸ maneno yangu.“

Mazungumzo baina ya Rashidi na Amina yalisita kwa muda, walibakia katazamana tu huku wamekamatana mikono. Kimya kilitawala kwa muda lakini Amina alikivunja kimya hicho na kusema, „Kama unanipenda kweli Rashidi kwa nini hutaki kuja kuniposa?“

„Sikiliza Amina,“ Rashidi alianza kusema, „si kama mimi sitaki kuja kukuposa lakini hali ya maisha ni ya taabu. Ijapokuwa nafanya kazi lakini kipato changu ni kidogo sana, hiyo kazi yenyewe haina dhamana, mtu anaweza kufukuzwa saa yoyote ile. Hivi juzi tu wenzetu chungu nzima walifukuzwa bure bila ya sababu,“ aliendelea.

„Si suala la kipato Rashidi,“ Amina alianza taratibu kabisa, „ni suala la masikilizano³⁹ baina ya watu wawili wapendanao. Nimi niko tayari kuolewa na wewe, shida au raha tutakuwa pamoja mimi na wewe. Mimi ni mtoto wa kimaskini kwa hivyo maisha nayaelewa vizuri.“

³⁸ „Amina“ bedeutet „trustworthy, honest“, „amini“ „trauen, vertrauen, glauben“: ein Wortspiel.

³⁹ Von „kusikilizana“ „gegenseitig zuhören“ abgeleitet.

Mazungumzo baina yao yalikuwa marefu, mpaka wakasahau kama usiku ulikuwa mwingi. Hata walipotanabahi ilikuwa saa tano za usiku. Amina aliondoka kwa haraka na kwenda nje.

Rashidi alikuwa bado anahisi homa kwa hivyo alijinyosha kitandani na kujivutia shuka lake, moja kwa moja mpaka asubuhi. (*Uk. 132-133*).

Am Sonntag darauf fahren Rashidi und Salum mit dem Fahrrad zu Mzee Farhani⁴⁰, der Rashidis Heiratsgesuch bei Mzee Dau, Aminos Vater, vorbringen soll. Beide werden von Mzee Farhani freundlich empfangen und verbringen den ganzen Tag dort. Mzee Farhani freut sich über Rashidis Vorhaben, besucht Mzee Dau, bespricht den Vorschlag und findet dessen Zustimmung, muß aber noch zwei Tage warten, bis die Angelegenheit mit der Verwandtschaft besprochen ist. Der Heiratsantrag wird angenommen und Rashidi verständigt.

Siku ya arusi ilifika⁴¹. Ukumbi wa nyumba ya kina Amina ulijaa watu. Ilikuwa ni wakati wa alasiri na watu wote ukumbini pale walikuwa wakimngojea bwana arusi. Rashidi alifika baada ya muda mfupi akifuatana na Faraji, Salum na Farhani. Wote walikaa katikati ya watu walioalikwa kwenye sherehe ile na mbele yao alikaa shekhe (shehe) muozaji. Shekhe huyo alivaa kizbao chenye ukosi shingoni, kanzu nzuri na kichwa chake kilikuwa kimezongorezwa kilemba cheupe. Baina ya shekhe yule na Rashidi palikuwa na kinara kilichokuwa na chetezo kilichokolezwa moto ya makaa, palikuwa na mrashi wa fedha na mkakasi mdogo wa fedha vile vile uliojaa ubani.

Shekhe yule aliandikaandika ndani ya buku (kitabu) lake la kuozea na baadaye alimshika mkono Rashidi na kumwambia, „Rashidi bin Majaliwa.“

Rashidi alinyamaza kimya akibakia kumtazama yule shekhe.

„Itikia ‚naam‘,“ shekhe alimuamuru Rashidi.

„Naam,“ Rashidi aliitikia.

„Umekubali kumuoa Amina binti Dau kwa mahari ya shilingi mia tatu?“ Rashidi aliduwaa tena na kumtazama shekhe machoni.

„Sema, ‚nimekubali,‘ “ shekhe alimuamuru tena Rashidi.

„Nimekubali,“ Rashidi alijibu.⁴²

Mara yule shekhe alimgeukia Mzee Dau aliyekuwa amekaa pembeni mwa Rashidi na kumtaka ampe mkono Rashidi na kumwambia, „Nimekubali kukuoza binti yangu Amina binti Dau kwa mahari ya shilingi mia tatu.“

Baada ya hapo Rashidi alitia sahihi karatasi ya kuolea, na Faraji na Salum walitia sahihi kama ni mashahidi. Mzee Dau alitia sahihi kama ni mzee mtoaji idhini.

Yalipomalizika hayo ulitiwa ubani uliotapakaza moshi ulionukia vizuri ukumbini pale na hapo tena ilipigwa fat-ha. Baadaye watu walinyunyiziwa marashi na kufukuziwa moshi wa ubani. Paliandaliwa halua na kahawa na baada ya kumalizika kila kitu Rashidi alisimama nje na kupewa mikono na wata waliohudhuria sherehe ile. Ilipofika zamu ya Mzee Dau kutoa mkono alimkamata Rashidi mkono na kumbinya huku akimwambia,

⁴⁰ *Farhan* bedeutet *glad, happy, cheerful, delighted*

⁴¹ Eine ähnliche Beschreibung ist im Roman *Kiu* auf Seite 84 zu lesen, auf dieser Website in *Matini 31-40*, S. 23.

⁴² Die Braut wird nicht gefragt.

„Nimekuoza mwanangu, mkae kwa salama na masikilizano, awe mke mkeo, msikilizane mzae ndume na njike.“

Hapakuwa na sherehe kubwa kwa arusi ile. Palikuwa na taarabu ndogo wakati wa usiku Rashidi alipokwenda kuingia nyumbani.

Rashidi alikaa fungate ya siku saba na baada ya kumalizika fungate, alimchukua mkewe nyumbani kwake na hapo tena maisha mapya yalianza kwa Rashidi na Amina.

Ijapokuwa Rashidi na Amina hawakuwa na kitu, waliishi kwa furaha na masikilizano. Vijana wawili hao walipendana kwa dhati na pendo lao lilizidi kukua kila siku zilipoendelea. Walifahamiana mwendo na tabia na hapana hata mmoja aliyependa kumkera mwenzake. (*Uk. 144-145*).

Rashidi arbeitet weiter als Kuli, während die Arbeitslage sich immer weiter verschlechtert. Arbeiter werden willkürlich entlassen, mißhandelt, und der Lohn wird reduziert. Die Arbeiter organisieren sich wieder und planen mit einen zweiten Versuch, ihre Forderungen durchzusetzen. Bakari fährt nach Dar-es-Salaam, um von dort Unterstützung zu holen. Nach seiner Rückkehr wird eine Versammlung im Arbeiterlokal in Miembeni einberufen und der bevorstehende Streik ausgerufen.

Am folgenden Tag ist die Stimmung am Hafen sehr unruhig, da die Arbeiter eine sofortige Aktion verlangen. Sie wollen nicht arbeiten, sondern haben sich in Gruppen hingesetzt und diskutieren ihre Probleme. Herr George kommt und fordert die Arbeiter auf, ans Werk zu gehen. Einen Arbeiter, der George vorwirft, daß er sie wie kleine Kinder behandelt, nennt George „bloody fool“ (Kuli: 150). Der Arbeiter greift George an und wirft ihn zu Boden. Einige Arbeiter bilden einen Kreis um George und schreien: „Schlag ihn! Töte ihn! Ein schwacher Mann!“ Nach einiger Zeit jedoch beruhigt sich die Lage. George geht in sein Büro und die Arbeiter kehren zu ihrer Arbeit zurück.

Nach der Arbeit an diesem Tag nimmt Rashidi an einer Sitzung teil und kommt spät zurück. Da er von Zeit zu Zeit spät nach Hause kommt, ohne eine Erklärung dafür zu geben, ist Amina sehr um ihn besorgt, doch auch zornig auf ihn.

Rashidi alifika nyumbani saa sita za usiku, amechoka taabani. Alikaribishwa na Amina aliyekuwa amehamaki, amevimba kama bofu, kana (*auch kama*) kwamba angepasuka saa yoyote ile.

„Leo umezidi tena!“ Amina alianza kusema, „tokea saa uliyotoka kazini mpaka saa hivi! Ulikuwa wapi!“

Rashidi hakujibu kitu, alinyamaza kimya na kuingia chumbani. Lakini kunyamaza kimya kwake hakumsaidia kitu kwani Amina alimfuatia huko huko chumbani huku akiendelea na malalamiko yake, „mimi nasema na wewe, wewe unanifanya kama mwendawazimu ndiyo?“

Rashidi aligeuka nyuma na kumtazama Amina aliyekuwa amesimama mlangoni. Alitabasamu na kutaka kusema kitu lakini kabla hajawahi kusema Amina aliingia kati, „Unacheka nini? Unafikiri hayo unayoyafanya mazuri? Toka ulipotoka kazini magharibi mpaka sasa hivi, mwenzako nimo ndani ya nyumba peke yangu wewe basi unatokomea huko na starehe zako,“ Amina alisema huku midomo inatetemeka kwa hamaki.

„Starehe gani niliyonayo mimi?“ Rashidi alianza kusema kwa sauti ya chini, „starehe yangu kubwa niliyo nayo duniani ni kukaa kwangu na mke wangu, basi, sina starehe nyingine.“

„Wacha kunizuzua mie bazazi mkubwa we, nakuona tu siku zote hizi, ukisharejea kazini hapo hapo unatoka tena mpaka saa uzitakazo, leo nd’o hukurudi kabisa mpaka saa hizi, lakini haidhuru shika uzi huo huo, yatakufalia mwenyewe hayo.“

Hapo tena Amina aliondoka pale mlangoni na kumwacha Rashidi chumbani anabadili nguo. (Uk. 151-152).

Nach dem Essen gehen sie schlafen. Dort sind sie in der Lage, in Ruhe miteinander zu sprechen. Rashidi beschreibt Amina die Lage der Arbeiter und erklärt ihr deren Forderungen. Sie zeigt Verständnis dafür. Sie versteht aber nicht, was ein Streik bedeutet und auch nicht, warum man nicht arbeitet, da alle doch so dringend Geld brauchen.

Die Hafenarbeiter drängen mehr und mehr auf Aktion. Bakari und seine Mitarbeiter haben ihre Forderungen bereits formuliert und die Flugblätter sind ausgeteilt worden. Sie enthalten die fünf folgenden Forderungen: Lohnerhöhung, fixe Arbeitszeit, zusätzliche Bezahlung für Überstunden, Arbeitsvertrag und Sozialversicherung. Dem Arbeitgeber wird eine zweimonatige Frist gewährt, diese Forderungen zu erfüllen, sonst drohen die Arbeiter mit neuerlichem Streik.

Amina äussert einen seltenen Wunsch an Rashidi.

Ilikuwa siku ya Ijumaa. Baada ya kurejea kazini na kupumzika kidogo, Rashidi alikuwa amekaa na mke wake wanakula chumbaai mwao. Rashidi alikuwa anafikiri kumwambia Amina habari ya mgomo wao kesho lakini kabla hajawahi kufanya hivyo kwa ghafla Amina alimwambia Rashidi, „Bwana, leo zimepita kanga nzuri za embe zinatembesha, zinatoka kwa Miwani mdogo, jina lake kibaya chako si chema cha mwenzako⁴³, kanga nzuri hizo,“ alisema Amina kwa kutilia mkazo sifa ya kanga hizo, „mji wake mweupe na zina pindo jekundu la makorosho, utanikatia bwana?“ aliuliza.

„Zinauzwa shilingi ngapi?“

„Shilingi kumi tu,“ Amina alijibu kwa haraka akihisi ombi lake limekwisha kukubaliwa. „Eeenh,“ Rashidi aliinamisha kichwa chini huku akifikiri. (Uk. 158).

Rashidi kann es sich nicht leisten, dieses Kanga für Amina zu kaufen, was für sie beschämend ist, wenn sie andere Frauen in der Umgebung trifft. Sie merken, dass sie immer die gleichen Kleider trägt. Das Gespräch wird unterbrochen durch Faraji, der um Einlass bittet. Er lädt Rashidi zu einer Sitzung ins Büro des Hafenarbeitervereins ein. Rashidi stimmt zu. Amina ist wütend. Sie ist nicht gut auf Faraji zu sprechen, denn sie gibt ihm die Schuld, dass es Rashidi schlecht geht.

„Nimejua mimi, madhali kaja yule shetani mwenzako lazima utatoka,“ Amina alisema huku matone ya machozi yanaanza kumdongoka, „lakini leo bora ulale huko huko manake mimi sitakufungulia mlango utakaporejea! Au bora unirejeshe kwetu kama umechoka na mimi!“ Amina aliendelea kusema. (Uk. 159).

⁴³ Die *Kangas* sind gewöhnlich mit einem Sprichwort versehen, nach dem sie auch benannt werden. In diesem Fall lautet es: „*Kibaya chako si chema cha mwenzako.*“

Rashidi kommt spät nach Hause und legt sich schlafen. Frühmorgens versucht er seiner Frau die Lage der Hafendarbeiter zu erklären.

Rashidi aliinua kutoka kitandani na kusimama, alimtazama Amina ambaye alikuwa bado amelala na halafu alimwamsha.

„Amina, Amina leo tuna mgomo huko banadarini,“ alijaribu kumwambia. Lakini Amina alikuwa bado ana usingizi na hakusikia aliyoambiwa na Rashidi.

„Unasemaje?“ Amina aliuliza huku akijinyosha.

„Nasema leo tuna mgomo huko gatini.“

„Mgomo wa nini?“

„Kwani wewe hujui nini mgomo?“

„Aa, mimi sikupata kuyasikia mambo hayo.“

„Kwa kifupi, leo tunakwenda kazini lakini hatutafanya kazi, hatutaki kufanya kazi.“

„Ala!“ Amina alishangaa na kutumbua macho, „kwa nini hamtaki kufanya kazi?“

„Tumechoka mateso na safari hii tumeazima kugoma mpaka tujue moja - ama tufanikiwe au sote tufukuzwe kazini.“

„Lakini si vibaya hivyo? Mnafikiri mkifukuzwa kazini mtafanya nini? Maisha yenyewe ya taabu, halafu mtu awe hana kazi si shida hiyo?“

Rashidi hakumjibu kitu, alimtazama na papo hapo alitoka na kwenda zake gatini. (*Uk. 161-162*).

Die Firma Smith Mackenzie nimmt diese Forderungen nicht zur Kenntnis. Nach Ablauf der Frist führen die Arbeiter ihre Drohung aus. Sie gehen zwar zum Hafen, arbeiten aber nicht. George und andere Angestellte sind gekommen und geben ihnen Weisung, die Arbeit aufzunehmen. Sie verweigern den Gehorsam. George holt die Polizei, die vom gleichen Offizier geführt wird, der den Angriff auf das Vereinslokal in Miembeni leitete. Er sieht Rashidi, der in der vorderen Reihe steht und erkennt ihn als denjenigen, der die Aktentasche Bakaris entwendet hatte.

Hapo tena yule afisa wa Kiingereza aliwaamuru askari wale kusimama msimamo wa kuwa tayari na marungu yao mikononi na mara ilisikika sauti ikisema kutoka kwenye kipaza sauti huko nje ya gari. „Wafanyakazi nyote mnatakiwa mwende kazini kwenu kwa haraka.“

Kwa muda kulikuwa kimya kisha sauti ile ilisikika tena na tena na kila mara ilikuwa ikisema kwa nguvu zaidi kuliko mwanzo (mwanzoni). „Wafanyakazi nyote mnatakiwa mwende kazini kwenu kwa haraka,“ lakini hakuna hata kuli mmoja aliyejali.

Hapo tena yule afisa wa Kiingereza alianza kuranda mbele ya makuli wale waliokuwa bado wamesimama na alipokuwa mbele, „We! Kuja hapa!“ alimwita.

Rashidi alinyamaza kimya huku akimtazama tu.

„Nasema wewe kuja hapa!“ alimwita tena kwa kelele.

Rashidi hakujibu kitu.

„Mimi naita wewe tokea wakati ule ...“ alisema yule afisa huku akimkunja Rashidi shati kifua na kutishia kumpiga.

Hapo Rashidi alijing'ang'anua na alipohisi afisa yule wa Kiingereza anazidi kumbinya ilimtoka ngumi kubwa na kumpiga afisa yule. Hapo hapo yule afisa aliwapa amri wale askari kushambulia na askari wale wakaanza kuwatandika makuli marungu. Sasa makuli iliwabidi wajitete. Ilikuwa pata shika na mapambano yalikuwa makali sana. Yule afisa wa Kiingereza alijisitukia amekabiliana uso kwa uso na Rashidi na alipopata kuinua

mkono wake tu kumpiga, Rashidi alimuwahi akamtandika konde kubwa. Hakuwahi kukaa sawa alimtandika konde la pili na hapo tena afisa yule aliangukaa chini na bila ya kuchelewa Rashidi alimchupia kifuani na kuanza kumkaba roho. Wale askari walivyoyaona yale walimzunguka Rashidi na wawili wakamkamata. (Uk. 164-165).

Rashidi wird verhaftet und eingesperrt.

Amina hakujua wapi akamtafute mumewe na mwisho alihisi bora afanye kila njia amtafute Faraji akiwa na hakika kabisa kwamba yeye atajua alipo Rashidi. Amina hakujua nyumba ya Faraji. Kutwa nzima aliranda mitaani, akaingia kila nyumba kuuliza. Karibu na usiku ndipo alipogundua nyumba ya Faraji. Alifika hapo kiasi cha saa moja na nusu usiku na baada ya kubisha hodi tu hakusubiri hata kujibiwa. Aliingia moja kwa moja mpaka ndani huku uso wake umesawajika. Faraji alistuka alipomwona Amina amemsimamia mbele yake; alikwisha jua lililompeleka pale.

„Yuko wapi Rashidi?“ Amina aliuliza, pumzi zake ziko juu juu.

Faraji aliinama chini halafu akainua uso wake na kumtazama Amina, aliinama tena chini na kabla hajawahi kuinua uso wake juu tena Amina alimuuliza tena, „Yuko wapi Rashidi? Tena usidanganye man’ake nimekwisha sikia habari za ghasiya (ghasia) zilizotokea huko kazini kwenu!“

„Rashidi kakamatwa,“ Faraji alilijibu kwa sauti ya unyonge.

Amina alimtazama Faraji kwa macho makali kama kutaka kumfahamisha kwamba yeye ndiye aliyemtaka yale. Macho yake yalianza kuelea ndani ya machozi na mara machozi haya yakaanza kumiminika taratibu na kutambaa juu ya mashavu yake. Hapo tena Amina hakuweza kujizuia, alianza kupiga mayowe, „Masikini mume wangu! N’na nani mimi tena! Ameniacha hali hii mja mzito. Masikini mume wangu!“

Faraji hakujua la kufanya. Alishangaa huku akibaki kumtumbulia macho Amina na kujaribu kumpoza.

„Sikiliza Amina, usilie, nyamaza; mume wako hakukamatwa kwa kuiba wala kwa kufanya jambo lolote lililo la aibu, Rashidi amekamatwa kwa sababu amesimama katika msingi wa haki. Yeye ni shujaa, jabari na wafanyakazi wote wa bandarini wana heshima kubwa kwake. Nenda zako nyumbani na kesho au keshokutwa mimi nitakuja kuonana na wewe na tutazungumza zaidi.“ (Uk. 166-167).

Die Regierung verschärft die Sicherheitsmaßnahmen und verbietet alle Versammlungen. Der Arbeiterverein versucht den Streikenden finanzielle Hilfe zu leisten und auch Amina bekommt ihren Anteil. Die Frauen sympathisieren mit den Hafendarbeitern und unterstützen den Kampf auf ihre Weise. Eines Tages besucht Faraji die Frauen, die Essen an die Hafendarbeiter verkaufen.

Faraji alimwita mmoja katika wale kina mama wanaouza chakula pale chini ya miti lakini kabla hajawahi hata kuagiza kile alichokitaka yule mama alianza kumvaa kwa masuala, „Mko wapi baba siku hizi? Tunajua kama mna mgomo lakini hata hamtupitii kuja kutuuliza hali?“

„Matatizo mama, matatizo,“ Faraji alijibu huku akivua kofia yake na kujipapasa kichwa.

„Ntilie muhogo, sahani moja.“

„Muhogo mtupu, samaki hutaki?“

„Pesa hazitimii mama, ntilie muhogo mtupu.“

Yule mama alijifunga kanga yake vizuri kiunoni huku akitabasamu, „Nitakupa na samaki japo kuwa huna pesa. Sikukopeshi, nakupa tu kwa mapenzi yangu mwanangu.“ „N’ tashukuru mama.“

„Tokea siku mliogoma biashara imepungua sana mwanangu,“ alianza kueleza yule mama, huku akipakua muhogo, „mimi nilikuwa nikiuza sufuria nne mpaka tano kutwa lakini siku hizi hata sufuria tatu hazimaliziki. Lakini haidhuru shikeni uzi huo huo kwani mkifanikiwa nyinyi ndiyo tumefanikiwa, sisi sote hapa tuko pamoja na nyinyi.“

Yule bibi alijaza sahani muhogo akatia vipande viwili vya samaki na kupelekea Faraji. Baada ya kuweka sahani ile aliinama na kumnon’oneza Faraji. „Sisi tunataka sana kukusaidieni lakini hatuna cha kukupeni, hali ya maisha unajua tena hutaki kuambiwa lakini mwenzenu yoyote (yeyote) atakayekuwa na haja ya chakula anaweza kuja hapa na kula shibe yake na huo ndiyo msaada tunaoweza kutoa kwenu.“

Faraja alishangaa. Hakufikiria kama kina mama wale wanaopigizana nao kelele kila siku kwa upungufu wa senti tano tu katika malipo wataweza kuwa na moyo kama ule.

„Ahsante, nitawaambia.“

Faraji alikula mbio mbio na baada ya kumaliza alianza safari yake ya kumtafuta Bakari. (171-172).

Nach einem langen Gespräch fährt Bakari nach Dar-es-Salaam und sucht nach Unterstützung bei den Hafendarbeitern dort. Er bleibt drei Tage und kehrt danach nach Sansibar zurück. Er bringt auch viele Flugblätter mit. Faraji besucht die Frauen, die Essen verkaufen und macht ihnen einen Vorschlag. Sie sollen die Speisen in diese Flugblättern einwickeln und sie so an die Arbeiter verkaufen. Auf diese Weise würden sie heimlich verteilt. Die Frauen stimmen zu.

Trotz des Verbotes versammeln sich die Arbeiter wieder im Vereinslokal. Bakari steigt auf einem Tisch und hält eine Ansprache. Plötzlich sind sie von allen Seiten von bewaffneten Polizisten umringt. Diese greifen die Arbeiter an.

Bakari alikuwa amesimama palepale juu ya meza hakuwahi kuteremka chini, „Jiteteteeni! Jiteteteeni!“ Bakari alipiga kelele kwa kadiri alivyoweza kuitoa sauti yake.

Sasa ulianza mvurugano. Watu wale waliokuwa wamejaa hasira waliwavamia askari. Kabla Bakari hajateremka pale juu ya meza askari mmoja alifika chini ya ile meza na kumtupia Faraji tako la bunduki. Faraji alidaka ile bunduki na tahamaki Bakari alimpiga kidevu yule askari. Bakari alipogeuka upande wa pili kutaka kumsukuma askari aliyetaka kumvuta mguu, alipigwa risasi ya kifua na askari mwingine aliyekuwa amejibanza kichochoroni kwa mbali kidogo. Aliruka juu na alipoanguka alifikia juu ya mikono ya Faraji. Alipapatika na haikuchukua muda alinyoka sawasawa na kukata roho. (Uk. 185)⁴⁴.

⁴⁴ Eine der beim Hafendarbeiterstreik in Sansibar führenden Persönlichkeiten war ein gewisser Abbas Othman aus Tanganyika, der sich ca. drei Wochen vor dem Streik als Arbeiter bei der *African Warfage Company* in Sansibar unter dem falschen Namen „Jomo Kenyatta“ anstellen hatte lassen. Dieser historische Othman hat Ähnlichkeiten mit Bakari im Roman Kuli. Der Autor gönnt seinem Bakari den Heldentod, der zu seinem Roman *à la thèse* paßt. Der historische Abbas Othman soll nach Beendigung des Streiks nach Dar-es-Salaam geflüchtet sein. Es scheint, daß er am frühen Morgen des

Faraji greift den Polizisten an, der Bakari getötet hat und auch er erleidet das gleiche Schicksal: er wird durch einen Kopfschuß getötet. Die anwesenden Arbeiter und Frauen aus der Nachbarschaft verwenden Möbelstücke, Brennholz und Küchengeräte als Waffen und bekämpfen die Polizei, können sich aber nicht auf die Dauer wehren. Die Polizei nimmt die Leichen in ihren Wagen mit und zieht ab.

Hunger, finanzielle Not und Arbeitslosigkeit zwingen die Arbeiter, die Arbeit wieder aufzunehmen. Rashidi ist immer noch eingesperrt. Nach drei Monaten wird er vor Gericht gestellt. Der Gerichtssaal ist voll, auch Amina ist gekommen, die Verhandlung zu beobachten. Rashidi, der sich zum Islam bekennt, schwört (kula yamini) auf den Koran.

Baada ya Rashidi kumaliza kula yamini yule hakimu alianza kusema kwa Kiingereza na mkalimani alitafsiri, „Rashidi bin Majaliwa, anashitakiwa kwa kuzusha ghasiya (ghasia) huko bandarini, ghasiya ambazo zilisababisha vita na kuumizwa maafisa na askari wa serikali.“

„Mimi nalikataa shtaka hilo,“ alisema Rashidi huku akionyesha hana wasiwasi hata kidogo.

Hapo tena alisimama afisa mmoja wa polisi na kuanza kuongoza mashtaka.

„Rashidi bin Majaliwa, umri wako miaka mingapi?“ aliuliza yule afisa aliyeongoza mashtaka.

„Ishirini na tano (mitano).“

„Unakaa wapi?“

„Gulioni.“

„Umezaliwa wapi?“

„Unguja.“

„Umeoa?“

„Ndiyo.“

„Una watoto?“

„Nimemwacha mke wangu na mimba.“

„Rashidi bin Majaliwa, unakumbuka siku ya Ijumaamosi (Jumamosi⁴⁵), tarehe 12, Machi mwaka huu, huko gatini, ulianzisha ugomvi uliosababisha kuumizwa kwa askari na maafisa wa polisi?“

„Mimi sikumbuki kuanzisha ugomvi na ikiwa nimefikishwa mbele ya mahakama haya kwa sababu ya kuanzisha ugomvi huko gatini basi napenda mjue kwamba mnamshitaki mtu siye, walioanzisha ugomvi ni hao maafisa na askari mnaosema wameumizwa kwa hivyo wao nd’o wanastahiki kufikishwa mbele ya mahakama hii na kujibu shtaka hilo.“

Hapo ulisikika mngurumo wa sauti za watu waliokuwemo mahakamani humo zikisema, „Kweli! Kweli tupu anayosema (anayoyasema) kijana huyo!“

Yule hakimu alinyanyua nyundo ya bao iliyokuwa pembeni mwake na kuigonga kwa nguvu juu ya meza yake huku akisema, „Hapana ruhusa kufanya ghasia mahakamani na mtu yeyote atakayefanya ghasia nitamtia ndani miezi mitatu kwa kosa la kuidharau mahakama.“

Tages, an dem die Arbeiter der *Warfage Company* zur Arbeit zurückkehrten, an Bord eines Dampfers, der nach Dar-es-Salaam fuhr, gesehen wurde.

⁴⁵ „mosi“ ist ein altes Wort für „moja“. *Juma-mosi* = Der erste Tag der Woche nach dem Freitagsgebet.

Kimya kilirudi na kesi ikaendelea. Kiongozi wa mashtaka aliendelea na masuala yake.
„Wewe Rashidi bin Majaliwa unakataa kama hukusababisha ghasiya huko gatini mpumbavu wewe?“
„Tafadhali usiniite mpumbavu,“ Rashidi alisema taratibu.
Hapa tena kiongozi wa mashtaka alimgeukia hakimu na kumwambia, „Mheshimiwa, naomba kesi iahirishwe mpaka wiki ijayo na mshtakiwa arejeshwe kizuizini bila ya kupata dhamana.“

Hapo tena yule hakimu alisema kwa Kiingereza na mkalimani alitafsiri, „Kesi inaahirishwa mpaka siku ya Ijumaatano (Jumatano) wiki ijayo.“ (Uk. 187-188).

Am vorgesehenen Tag wird das Verhör wieder aufgenommen.

Kiongozi wa mashtaka aliendelea kumhoji Rashidi.
„Rashidi bin Majaliwa.“
„Naam.“
„Unakumbuka kama wewe umekula yamini kama utasema kweli?“
„Nakumbuka.“
„Mbona juzi umetwambia uwongo?“
„Uwongo gani?“
„Kwamba wewe siye uliyeanzisha ghasia huko bandarini?“
„Mimi siye na aliyesababisha ghasia mnamjua vizuri.“
Hapo tena kiongozi wa mashtaka alipandwa na hasira na kuja juu.
„Wewe Rashidi sikiliza! Mimi nakutaka wewe useme kweli kwa faida yako mwenyewe! Unajua kwamba ukisema uwongo utapata taabu?“
„Mimi nasema kweli tupu. Na kwa taabu tu, mimi taabu siogopi, nimezaliwa katika taabu, nimelelewa katika taabu, taabu ndiyo iliyonilea,“ Rashidi alisema huku akionyesha hamasa zimemjaa. (Uk. 189).

Der Kiongozi wa Mashtaka kommt auf die Anklage zu sprechen.

„Unakumbuka kama ulimpiga ngumi afisa wa polisi siku hiyo ya ugomvi.“
„Nilimpiga ngumi baada ya yeye kunivamia na kuanza kunikaba.“
„Mimi sitaki hadithi! Jibu kama ulimpiga au hukumpiga.“
„Siwezi kujibu hivyo, lazima ni(ku)elezee vile ilivyokuwa.“
„Wewe unajua kwamba kumshambulia afisa wa polisi ilihali amevaa yunifomu ni kosa kubwa sana?“
„Sasa ulitaka nimwache anipige tu kwa sababu amevaa yunifomu?“
„Wacha akuuliza maswali na jibu ninavyokuuliza! Unajua au hujui?“ Yule kiongozi wa mashtaka aliuliza kwa hamaki huku macho yote ameyatumbua. Rashidi alisita kidogo huku akifikiri la kujibu.
„Jibu upesi! Unajua au hujui?“ yule Kiongozi wa mashtaka aliendelea kupiga makelele.
„Najua,“ Rashidi alijibu.
„Kwa hivyo ulifanya kosa kumpiga afisa wa polisi ilhali amevaa yunifomu?“ kwa ghafla yule kiongozi wa mashtaka aliziteremsha hamaki zake na kumuuliza Rashidi taratibu.
„Sikufanya kosa lolote.“
„You! Mpumbavu! Sasa hivi umesema unajua kwamba ukimshambulia afisa wa polisi ilhali amevaa yunifomu ni kosa kubwa halafu umesema wewe hukufanya kosa kumshambulia afisa wa polisi huko gatini?“ hapo kiongozi wa mashtaka alizipandisha tena ghadabu zake na kuongezeka kelele.

„Mimi sikuanza kumshambulia, yeye ndiye aliyeanza kunishambulia na mimi nilikuwa nimo katika kujitetea nisije nikaumizwa.“ (Uk. 190-191).

Der Kiongozi wa Mashtaka möchte wissen, ob Rashidi irgendwelche rechtlichen Schritte unternommen hat.

„Nakuuliza tena, mlimuarifu mkuu wa kazi wa serikali kuhusu habari hiyo?“

„Mimi sijui mtu huyo,“ Rashidi alijibu.

„Humjui? Wewe hujui kama katika nchi yuko mtu anaitwa (anayeitwa) *Labour Officer*?“

„Sijui.“

„Wala hujui kama katika nchi ipo ofisi inayoitwa *Labour Office*?“

„Sijui.“

„Nini unachokijua basi?“

„Mimi najua kazi ya ukuli tu.“ (Uk. 193).

Der Kiongozi wa Mashtaka kommt auf die „ghasia“ und den Streik zu sprechen. Rashidi ersucht ihn, diesbezüglich die Polizei zu fragen. Die Verhandlung wird vertagt. Bei der nächsten Verhandlung tritt ein britischer Polizist William Davis (Davies) als Zeuge auf.

William Davis alikuwa Mzungu. Aliingia ndani na (ya) ukumbi wa mahakama akiwa amevalia sare yake ya polisi iliyokuwa safi na kupigwa pasi vizuri. Ilikuwa imenyoka kwa wanga iliyotiwa. Alipofika humo alipiga saluti kutoa heshima kwa hakimu na baada ya hapo kiongozi wa mashtaka alimtaka aingie kwenye kizimba cha mashahidi. Alikula yamini na hapo tena kiongozi wa mashtaka alianza kumhoji kwa lugha ya Kiingereza huku mkalimani akitafsiri.

„Bwana William Davis, unakumbuka nini kilitokea siku ya Ijumaamosi (Jumamosi) tarehe 12, Machi mwaka huu (1948) huko bandarini?“

„Nakumbuka,“ William alijibu.

„Unaweza kuieleza mahakama nini kilitokea siku hiyo?“

Hapo William Davis alisimama vizuri ndani ya kizimba. Kijasho chembamaba kilikuwa kinamtoka ijapokuwa mapankaboi yalikuwa yamefunguliwa yote mahakamani humo. Labda kwa sababu ya sare ya haki aliyovaa (aliyoivaa).

Alitoa kitambaa cheupe mfukoni na kujipangusa jasho na hapo alianza kusema, „Ilikuwa siku ya Ijumamosi⁴⁶. Ilikuwa tarehe 12. Machi mwaka huu. Nilikuwa nimekaa ofisini kwangu na mara nilipokea simu kutoka huko gatini na niliyezungumza naye aliniambia kwamba kuna fujo huko. Hapo hapo niliwaamuru askari kiasi cha thelatini kufuatana na mimi na baada ya muda tulifika gatini. Tulipofika huko tulikuta fujo iliyokuwa ikifanywa na makuli na sisi tulichukua hatua ya kutuliza fujo hiyo.“

„Ahsante, Bwana William,“ alishukuru kiongozi wa mashtaka, „unaweza kutwambia nani aliyeanzisha fujo hiyo?“ Kiongozi huyo wa mashtaka aliendelea.

„Mshtakiwa aliomo (aliyemo) kizimbani ndiye alieanzisha (aliyeanzisha) fujo hiyo.“

„Unaweza kuieleza mahakama vipi mshtakiwa alianzisha fujo hiyo?“ (Uk. 194-195).

⁴⁶ Mit der Rechtschreibung nimmt es der Autor nicht genau: Manchmal „ghasiya“, manchmal „ghasya“ und einmal „ghasia“, dann wieder „Ijumamosi“ ein anderermal „Jumaamosi“ und manchmal „Jumamosi.“ Gelegentlich verwendet er die Sansibar-Varianten, z.B. *kheri* statt *heri*, *ahsante* statt *asante*.

Der Polizeibeamte William Davis nimmt sich Zeit, den Schweiss abzuwischen, das Kopfhaar in Ordnung zu bringen, sich ein wenig zu erholen.

„Nilimwita mara ya kwanza hakuitika, nilimwita tena mara ya pili hakuitika na nilipomsogelea mbele yake kutaka kumuuliza kitu alinipiga na hapo tena ndipo fujo ilipoanza.“

Kiongozi wa mashtaka aligeuka na kumtazama Rashidi aliyekuwa amesimama kizimbani na halafu alimtazama William na kumuuliza, „Kwa hiyo unaihakikishia mahakama kwamba mshtakiwa ndiye aliyeanzisha fujo hiyo?“

„Ndiyo.“

„Ahsante Bwana William,“ Kiongozi wa mashtaka alishukuru na kukaa juu ya kiti chake. (Uk. 195).

Der Kiongozi wa Mashtaka fragt Rashidi, ob er Fragen an Herrn William Davis stellen möchte. Rashidi nimmt die Gelegenheit wahr.

„Ulipokuwa ofisini kwako ulipata simu na uliyezungumza naye alikwambia gatini kuna fujo?“

„Ndiyo,“ alijibu William.

„Mlipofika gatini wewe na askari wako, mlikuta fujo yoyote?“

William alitoa tena kitambaa na kujipangusa jasho huku akizipuna kwa nyuma nywele zilizokuwa zikimkera zinaporomoka kipajini. “Watu walikuwa wakifanya ghasiya,“ alijibu William.

„Walikuwa wakifanya ghasiya au fujo?“ Rashidi aliuliza.

„Ghasiya.“

„Mimi sikukuuliza habari ya ghasiya Bwana William, nimekuuliza (kama walikuwa) wakifanya fujo?“

„Ghasiya ndiyo fujo,“ alijibu William.

„Ghasiya siyo fujo Bwana William, ghasiya na fujo ni vitu viwili mbali mbali, ghasiya kila siku zipo gatini, mimi nakuuliza ulikuta fujo?“

William alikuwa anababaika hajui ajibu nini. „Sisi tulikuta watu wanafanya fujo hawataki kwenda kazini,“ alitafsiri mkalimani baada ya William kusema hivyo kwa Kiingereza kwa sauti ya mtu aliyekuwa na hakika kwamba amesema uwongo.

„Bwana William, kama unaweza kukumbuka, ulipoulizwa mwanzo (mwanzoni) ulisema mlipofika huko gatini mlikuta fujo au siyo?“

„Ndiyo,“ kwa ghafla William alijibu.

„Ina maana mlipofika nyinyi gatini fujo ilikuwa ishaanza?“

William hapo alianza kubabaika na mara alijibu kama mtu asiyekuwa na hakika anajibu nini, „Ndiyo.“

„Ikiwa mlipofika huko mlikuta fujo ishaanza ulijuaje kama mimi ndiye niliyeanzisha fujo hiyo?“ (Uk. 195-196).

Der Kiongozi wa Mashtaka unterbricht die Befragung.

„Nafikiri jambo muhimu ni kwa mshtakiwa kuithibitisha mahakama kama yeye hakumpiga Bwana William alipomwita.“ (Uk. 196).

Rashid nimmt zur Kenntnis, dass die Sache hin und her gedreht wird. Das Gericht vertagt sich.

Er bekommt einen handgeschriebenen Brief von seiner Frau in dem sie ihn die Treue verspricht, auch wenn er verurteilt werde.

Am Tag der letzten Verhandlung wird das Urteil gefällt.

„Kwa mujibu wa ushaidi uliofikishwa mbele ya mahakama hii, nimetosheka kwamba mshtakiwa, Rashidi bin Majaliwa alisababisha mapigano huko bandarini. Mshtakiwa pia ana hatia ya kushambulia kwa kumpiga afisa wa polisi. Kwa sababu hizi, Rashidi bin Majaliwa nakufunga miaka miwili kwa kusababisha mapigano na mwaka mmoja kwa kumshambulia afisa wa polisi kwa kumpiga. Kwa hivyo kwa makosa yako nakufunga miaka mitatu kazi ngumu.“

Baada ya kumaliza tu kutoa hukumu yake hakimu yule alinyanyuka na kwenda zake na watu wote waliokuwemo mahakamani mle walitoka wengi katika wao wakiwa na majonzi. Alipoteremka kutoka kizambani Rashidi alitiwa pingu na kuchukuliwa na askari mmoja mkono wake wa kulia na wa pili mkono wake wa kushoto na kutolewa nje. (Uk. 199).

Rashidi begegnet seiner Frau Amina.

Alipofika nje tu kwa bahati Rashidi alijiona amekabiliana uso kwa uso na Amina. Amina alianza kutokwa na machozi alipomwona mumewe na pingu mikononi. Rashidi nywele zilimsimama. Alisita na kumtazama Amina lakini mara askari wale walimburura. Alipokuwa akibururwa alitumia nguvu na kusita huku akigeuka nyuma kumtazama mkewe ambaye tumbo lake lilikuwa kubwa kwa mimba iliyokwisha pea (kupea) lakini alivutwa kwa nguvu na askari wale, „Twende huku! Unatazama tazama nini?“ Alisema mmoja katika askari wale.

Diese Szene einer zarten und innigen Liebe - die in der Swahili-Literatur sonst selten vorkommt - bildet den Abschluss eines im übrigen sonst so aggressiven Romans.

3. Kusimulia Kuli

Diese Nacherzählung ist für eine mündliche, sofortige Rückübersetzung bestimmt, kann aber auch für eine schriftliche Prüfung verwendet werden.

1. Majaliwa ist ein *Kuli* am Hafen von Sansibar.
2. Er hat mit dieser Arbeit angefangen, als er 21 Jahre alt war.
3. Jetzt ist er 55 Jahre alt und immer noch *Kuli*.
4. Er ist mit Bibi Mashavu verheiratet und hat einen Sohn, der Rashidi heißt.
5. Er ist ein Tagelöhner.
6. Er verbraucht den Lohn für die täglichen Bedürfnisse seiner Familie.
7. Er hat keine Ersparnisse und auch keine Sozialversicherung (*bima ya majaliwa*).
8. Ein Arbeiter hat einen Unfall.
9. Die Firma weigert sich, ihn ins Spital zu bringen.
10. Die Arbeiter sammeln Geld (*changa fedha*) und helfen ihm.
11. Majaliwa ist schwer krank.
12. Er stirbt.
13. Seine Frau ist Witwe und sein Sohn Waise.
14. Sie treiben Kleinhandel (*fanya biashara ndogondogo*) und leben davon.
15. Rashidi geht auf die Suche nach Arbeit.
16. So wie sein Vater will auch er *Kuli* werden.
17. Um 7.30 in der Früh steht er vor dem eisernen Tor am Hafen.
18. Hier regiert Gewalt (*mabavu* 6).
19. Rashidi kann mit den starken Männern nicht konkurrieren (*shindana na*).
20. Er bekommt Arbeit in einem Eßlokal am Straßenrand.
21. Er hilft kochen, auftischen (*pakua chakula*) und das Geschirr abwaschen.
22. Er bekommt kein Geld, aber dafür *ugali* und ein Gericht aus Erbsen (*kunde*)
23. Nach langer Zeit hat er nun Gelegenheit, sich satt zu essen.
24. Am folgenden Tag trifft er einen Nachbar, Mzee Tindo, der Arbeiter für die Firma CGA anstellt (*ajiri*).
25. Ein Inder namens Morarji ist der Manager (*Mkurugenzi*) dieser Firma.
26. Rashidi bekommt eine Arbeit mit Tageslohn.
27. Obwohl die Arbeit sehr schwer ist, versucht Rashidi sie fleißig zu verrichten.
28. Eines Tages findet Rashidi heraus (*gundua*), daß Mzee Tindo einen Teil der Lohnbeträge für sich behält, obwohl er ein Monatsgehalt bezieht.
29. Er reicht eine Beschwerde bei Mzee Tindo ein.
30. Mzee Tindo bittet die Arbeiter, zwei Vertreter zu wählen, die bei Herrn Morarji vorsprechen sollen.
31. Rashidi und Farjalla werden gewählt.
32. Mzee Tindo geht heimlich zu Morarji und warnt ihn.
33. Morarji hört zu, was Rashidi und Farjalla zu sagen haben und entläßt sie (*fukuza kazi*) sofort.
34. Rashidi hat zwei Monate lang keine Arbeit.
35. Bibi Mashavu gibt Rashidi ihre Goldkette.
36. Rashidi hinterlegt sie bei einem indischen Pfandleiher und borgt Geld aus.
37. Der Pfandleiher gibt Rashidi Tansania-Shilling (TS) 100,- dafür und verlangt monatliche Zinsen von TS 10,-.
38. Rashidi bekommt Arbeit am Hafen.
39. Er ist sehr stolz, daß er jetzt *Kuli* ist.
40. Eines Tages kommt ein Fremder mit einer Aktentasche aus Leder.
41. Er heißt Bakari.

42. Er geht in das Büro des Engländers Herrn George.
43. Dort diskutieren sie die Probleme der Arbeiter eine ganze Stunde lang.
44. Als sie das Büro verlassen, sind beide wütend.
45. Bakari gibt den Arbeitern einige Flugblätter.
46. Sie fordern bessere Arbeitsbedingungen für die Arbeiter.
47. Rashidi kann weder lesen noch schreiben.
48. Sie gründen eine Schule für Erwachsene.
49. Eines Tages erleidet ein Arbeiter namens Manafi einen Unfall.
50. Ein Zuckersack fällt vom Kran herunter und wirft ihn ins Meer.
51. Er ertrinkt.
52. Die Firma Smith Mackenzie befaßt sich mit dem Fall nicht.
53. Die Frau Manafis und seine drei Kinder sind nicht versichert (*hawana bima*).
54. Die Arbeiter versammeln sich in Miembeni.
55. Die Polizei dringt (*penya*) in das Haus ein und verhaftet Faraji und Bakari.
56. Rashidi nimmt die Aktentasche Bakaris und flüchtet.
57. Am folgenden Tag geht niemand am Hafen arbeiten.
58. Faraji und Bakari werden verhört und eingesperrt.
59. Sie werden ersucht, die Arbeiter zur Arbeit zurück zu bringen.
60. Sie lehnen dies ab.
61. Am dritten Tag werden sie freigelassen.
62. In der zweiten Woche sieht die Firma Smith Mackenzie ein, daß sie Verluste macht.
63. Es gibt eine grosse Sitzung im Saal des Hauptsitzes (*makao makuu*) der Firma beim Zollamt (*forodhani*).
64. Die Firma macht viele Versprechungen.
65. Sie hält ihre Versprechen nicht.
66. Die Arbeiter sind gezwungen, zur Arbeit zurück zu kehren (*kurudi kazini*), weil sie kein Geld mehr haben.
67. Eines Tages, als Rashidi bei der Arbeit ist, erhält er die Nachricht, daß seine Mutter erkrankt ist.
68. Er beeilt sich und kann seine Mutter noch kurz vor ihrem Tod sehen.
69. Rashidi wohnt allein und einsam.
70. Er lernt Amina kennen, die er früher im Hause Mzee Tindos gesehen hatte.
71. Damals trug sie ein *kanga* mit dem Spruch: „*Mpende akupendaye*“.
72. Für beide ist es die erste Liebe.
73. Als Rashidi einmal krank ist, besucht ihn Amina und sorgt für ihn.
74. Sie sprechen von Liebe und Ehe.
75. Rashidi besucht seinen Onkel Farhani und bittet ihn, bei Aminas Vater Mzee Dau um Amina zu werben (*kumposa Amina*).
76. Aminas Eltern stimmen zu.
77. Die Hochzeitsfeier ist einfach (*ya kawaida tu*).
78. Rashidi und Amina sind arm und (bzw. aber) glücklich (*wameridhika*).
79. Die Lage der Arbeiter am Hafen verschlechtert sich (*inaharibika*).
80. Sie fordern ihre Rechte.
81. Sie fordern fünf Dinge: Lohnerhöhung, fixe Arbeitszeiten, doppelten Lohn für Überstunden, Arbeitsvertrag und Sozialversicherung.
82. Sie geben der Firma zwei Monate Zeit, diese Forderungen zu erfüllen.
83. Nach sieben Wochen gehen die Arbeiter zur Arbeitsstelle, arbeiten aber nicht.
84. Ein Engländer, der mit afrikanischen Polizisten kommt, befiehlt den Arbeitern zur Arbeit zurückzukehren.
85. Sie weigern sich.
86. Der Engländer erkennt Rashidi, der die Aktentasche Bakaris versteckt hatte.

87. Er befiehlt ihm, nach vorne zu kommen.
88. Rashidi verweigert den Befehl.
89. Der Engländer wird wütend.
90. Es gibt eine Rauferei (*mafarakano*) zwischen den Arbeitern und der Polizei.
91. Rashidi wird verhaftet und eingesperrt.
92. Amina erfährt davon erst drei Tage später.
93. Sie schreibt ihm einen Brief.
94. Sie verspricht ihm die Treue.
95. Die Arbeiter helfen ihr finanziell.
96. Bakari fährt nach Dar-es-Salaam und holt Unterstützung von der dortigen Gewerkschaft.
97. Die Flugblätter, die Bakari gebracht hat, werden verteilt.
98. Als die Arbeiter sich versammeln, werden sie von der Polizei umringt.
99. Bakari wird von der Polizei getötet.
100. Auch einige Arbeiter werden erschossen (*pigwa risasi*).
101. Die Leichen werden von der Polizei abtransportiert (*hamishwa*).
102. Der Streik hat wenig Erfolg (*mafanikio madogo*).
103. Die Arbeiter kehren wieder zur Arbeit zurück, weil sie finanzielle Schwierigkeiten haben (*shida za kipesa*).
104. Rashidi wird zu einer Gefängnisstrafe von 3 Jahren verurteilt.
105. Amina möchte mit ihm sprechen.
106. Sie ist schwanger.
107. Er darf sich nicht von ihr verabschieden.

Tamati